# KRISTO ALIPENDA KANISA

par

**WILLIAM MACDONALD**

**Traduction G. Harlow**

Everyday Publications Inc.
310 Killaly St. West
Port Colborne, ON
Canada L3K 6A6

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

## MANENO YALIYO KITABUNI


| | |
|---|---|
| | *Ukarasa* |
| Kanisa, ndilo Mwili wa Kristo | 3 |
| Kanisa la pahali fulani | 11 |
| Kanisa la Kristo ni mwili mmoja | 13 |
| Kristo ni Kichwa cha mwili ndilo Kanisa | 16 |
| Waamini wote ni viungo vya mwili mmoja | 17 |
| Roho Mtakatifu katika Kanisa | 21 |
| Kuhukumu zambi katika Kanisa | 24 |
| Kuongezeka kwa Kanisa | 28 |
| Waamini wote ni makuhani | 33 |
| Ubatizo na Meza ya Bwana | 37 |
| Kusanyiko la maombi | 43 |
| Wazee | 48 |
| Watumishi | 53 |
| Mali ya Kanisa | 56 |
| Kazi ya wanawake | 61 |


*Imprimé au Canada*

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

# KANISA, NDILO MWILI WA KRISTO

"Kristo alivyopenda kanisa, na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake." Inatupasa sisi vilevile kupenda Kanisa na kujitoa kwa ajili yake kwa njia ya utumishi wetu wa furaha, ili Kanisa duniani liweze kusitawi na kuongezeka na kushinda.

Kusudi la kitabu hiki ni kuona maneno Agano Jipya linayofundisha juu ya Kanisa na kazi yetu ndani ya Kanisa lile na namna gani inapasa kuliongoza. Kwanza tutaangalia mafundisho juu ya "kanisa, lililo mwili wa Kristo." Kisha tutaangalia mafundisho ya Agano Jipya juu ya kanisa linalokutana kwa pahali pamoja.

Kwa mwanzo wa kitabu hiki tukumbuke ya kwamba kama tukitaka Kanisa kuwa taratibu inapasa kila Mkristo ndani yake kutembea taratibu mbele ya Bwana. Tutaona neno hili tena na tena katika kitabu hiki.

## 1. Sasa tuangalie kama Kanisa ni nini

**A. Katika Agano Jipya KANISA kwa Kiyunani ni *eklesia*,** maana yake watu wanaokwisha kuitwa kutoka katikati ya watu wengine wakutane pamoja. Stefano alitumika na neno hili katika Matendo 7:38 wakati aliposema juu ya Waisraeli jangwani. Lakini zaidi tunaona neno hili wakati waandishi wa Agano Jipya waliposema juu ya waamini waliokutana pamoja kuabudu Mungu. Hivi Paulo anasema juu ya "kanisa la Mungu ambalo alinunua kwa damu yake mwenyewe" (Matendo 20:28). Katika barua yake ya kwanza kwa Wakristo kwa Wakorinto, mtume Paulo anagawa watu wote duniani katika mafungu matatu, Wayuda, Wayunani, na kanisa la Mungu (1 Wakorinto 10:32). Tena anaita waamini wale ambao aliwatesa wakati asipookolewa bado na jina hili "**kanisa** la Mungu".



copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

**B.** **Kanisa ni kitu hai.** Ni watu wote wanaozaliwa tena na wanaokuwa na Roho Mtakatifu mioyoni mwao.

**C.** **Kanisa lina majina mengi mengine katika Agano Jipya.** Tuangalie majina haya kwa kutusaidia kufahamu vizuri kama kanisa ni nini.

1. Kanisa linaitwa **"KUNDI"** (Yoane 10:16). Kabila la Wayuda lilikuwa zizi. Kanisa ni kundi. Katika Yoane 10:16 Bwana Yesu alisema, "Na nina kondoo wengine, wasio wa zizi hili, sharti niwalete vile na watasikia sauti yangu; na watakuwa kundi moja, na mchungaji mmoja." Hivi neno hili KUNDI linatukumbusha ya kwamba Wakristo wanakaa pamoja na wanachungwa na mapendo na Mchungaji Mwema, wakisikia sauti Yake na wakimfuata.
2. Kanisa linaitwa vilevile **"SHAMBA LA MUNGU"** (1 Wakorinto 3:9). Kanisa ni shamba la Mungu na ndani yake anataka kupata matunda kwa utukufu Wake. Hivi jina hili linatukumbusha maneno ya kuzaa matunda kwa Bwana.
3. Kanisa linaitwa vilevile **"JENGO LA MUNGU"** (1 Wakorinto 3:9). Neno hili linatuonyesha ya kwamba Mungu ana kazi ya kujenga. Anaongeza mawe hai kwa Kanisa Lake. Inafaa tutoe maisha yetu kwa kazi hii ya kujenga Kanisa Lake kwani Yeye Mwenyewe anaweka roho sana juu yake.
4. Linaitwa vilevile **"HEKALU LA MUNGU"** (1 Wakorinto 3:16). Jina hili linatukumbusha mara moja maneno ya kuabudu, na ya kwamba Mungu anaabudiwa tu na wale walio katika Kanisa Lake wakati wa sasa.
5. **"MWILI WA KRISTO"** (Waefeso 1:22,23). Kwa njia ya mwili wake mtu anaonyesha mafikili na makusudi yake. Hivi Kristo alichagua Kanisa kwa kujionyesha ndani yake kwa dunia leo. Wakati tunapofahamu neno hili, hatutafikili tena ya kwamba maneno ya Kanisa ni kitu kidogo, lakini tutajitoa kabisa kwa kusaidia mwili wa Kristo, ndilo Kanisa kwa njia yo yote tunayoweza.
6. **"MTU MPYA"** (Waefeso 2:15). Jina hili linatukumbusha maneno ya kuzaliwa tena. Sasa katika Kanisa hatufikili

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

tena ya kwamba wengine ni Wayuda na wengine Mataifa, lakini Mungu anakutanisha makabila yale kuwa mtu mpya mmoja katika Kristo.

7. **"KAO"** (Waefeso 2:22). Jina hili linatuonyesha ya kwamba Mungu anakaa katika Kanisa sasa. Hakai katika hema au hekalu ndilo jengo la dunia, kama wakati wa Agano la Kale.

8. **"BIBI-ARUSI"** (Waefeso 5:25-27; 2 Wakorinto 11:2). Jina hili linatukumbusha zaidi juu ya mapendo. "Waume, mupende wake wenu, kama vile Kristo alivyopenda kanisa, na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake; apate kulitakasa, akiwa amelisafisha kwa maji katika neno; apate kulijiletea mwenyewe, kanisa la utukufu, pasipo alama wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi; lakini liwe takatifu na pasipo kilema." Kama Kristo alivyopenda Kanisa na kujitoa kwa ajili yake, inapasa Kanisa kujaa na mapendo Kwake kama bibi-arusi alivyo na mapendo kwa Bwana yake.

9. **"NYUMBA YA MUNGU"** (1 Timoteo 3:15). Nyumba inatuleta kufikili juu ya utaratibu na hukumu kwa maneno yasiyo taratibu. Tunaona neno hili katika 1 Timoteo 3:15 vilevile, "upate kujua sana namna ilivyokupasa kutenda katika nyumba ya Mungu." Tunaona maneno ya hukumu katika 1 Petro 4:17, "wakati umefika kwa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu."

10. **"NGUZO NA MSINGI WA KWELI"** (1 Timoteo 3:15). Kwa wakati wa zamani nguzo haikuwa na kazi ya kubeba nyumba tu, lakini mara nyingi watu walitumika nazo kwa kufunga matangazo yao juu yao. Hivi tunaona ya kwamba Mungu alichagua Kanisa kubeba na kutangaza kweli Yake, na tunaweza kusema ya kwamba Wakristo wale wanaofanya kweli mapenzi ya Mungu na kutimiza makusudi Yake ni wale ambao wanajitoa kabisa kwa kuongeza Kanisa na kulisimamisha imara.

Watu wengi leo wanasema ya kwamba kazi yao ni kuhubiri Habari Njema, na hawafikili zaidi maneno ya Kanisa. Lakini

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

tukumbuke ya kwamba kazi ya mtume Paulo ilikuwa na sehemu mbili:

1. "Nilipewa neema hii ya kuhubiri Mataifa utajiri wa Kristo usiotafutikana," na vilevile

2. "kutangazia watu wote wajue habari za madaraka ya siri iliyofichwa tangu zamani ndani ya Mungu," ndiyo kuwasimamisha katika maneno makubwa ya Kanisa. Ona Waefeso 3:8,9.

## 2. Mwanzo wa Kanisa

**A.** Walimu wa Neno la Mungu wana mawazo mbalimbali juu ya neno hili. Wengine wanaamini ya kwamba mwanzo wake ulikuwa kwa wakati wa Israeli katika Agano la Kale. Wengine wanasema ya kwamba kwa wakati wa Agano la Kale Kanisa halikuwa lakini ya kwamba lilianza nyuma ya mauti ya Kristo. Tuonyeshe kwa sababu gani wanafikili hivi:

1. Katika **Waefeso 3:4,5** Paulo alisema ya kwamba kanisa ni "siri" isiyojulishwa kwa wana wa watu wa vizazi vingine, kama ilivyofunuliwa sasa kwa mitume yake watakatifu na manabii katika Roho. Tena katika shairi 9 anasema ya kwamba Kanisa ni "siri iliyofichwa tangu zamani ndani ya Mungu." (Ona vilevile Wakolosayi 1:26 na Waroma 16:25,26.) Hivi Kanisa lilikuwa siri ya Mungu kwa wakati wa Agano la Kale na siri hii haikufunuliwa kufika wakati wa mitume na manabii ya Agano Jipya.
2. Katika **Matayo 16:18** Bwana Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitajenga kanisa langu." Au kusema wakati Yesu alipokuwa duniani, Kanisa halijakuwa bado.
3. Tena katika **Waefeso 4:8-11** Paulo anaonyesha ya kwamba Kristo aliwapa Kanisa zawadi nyuma ya kufufuliwa Kwake toka wafu na nyuma ya kwenda Kwake mbinguni. Basi kama Kanisa lingalikuwa mbele ya saa ile kama lisingalikuwa na walimu na wahubiri kwa kulijenga.

**B.** Tunaweza kuonyesha ya kwamba Kanisa lilianzwa siku ya Pentekote.

1. Tunasoma ya kwamba mwili wa Kristo ulifanywa kwa njia

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

ya ubatizo wa Roho Mtakatifu (1 Wakorinto 12:13). Basi tunaweza kujua wakati gani ubatizo huu wa Roho Mtakatifu ulitokea?

2. Katika Matendo 1:5, saa ndogo tu mbele ya kwenda kwa Bwana Yesu mbinguni aliahidi mitume, "mutabatizwa katika Roho Mtakatifu nyuma ya siku si nyingi."
3. Siku ya Pentekote, "wakajazwa wote Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine kama Roho alivyowapa kusema" (Matendo 2:4).
4. Wakati tunapofika kwa Matendo 5:11, tunaona Kanisa linakwisha kuzaliwa, kwa sababu tunasoma ya kwamba "woga mkubwa ulipata kanisa pia."

Maneno haya yanaonyesha ya kwamba siku ya Pentekote ilikuwa siku ya kuzaliwa kwa Kanisa.

## 3. Maneno makubwa saba juu ya Kanisa

Katika Matendo ya Mitume na barua za Agano Jipya tunapata maneno mingi juu ya Kanisa la Mungu. Hapa tutataja maneno saba tu na tutaongeza kusema maneno mengine juu yao nyuma.

**A. KUNA MWILI MMOJA (**Waefeso 4:4).

Maandiko Matakatifu yanafundisha ya kwamba kuna Kanisa moja tu. Hata kama maneno tunayoona duniani hayapatani na neno hili, kwa macho ya Mungu kuna mwili mmoja tu wa waamini hapa duniani wakati wa sasa. Hata kama haiwezekani kwetu kuona Kanisa lile zima pamoja, Roho Mtakatifu analifanya kuwa mwili mmoja.

**B. KRISTO NI KICHWA CHA MWILI** (Waefeso 5:23; Wakolosayi 1:18).

Paulo anatumika hapa na mwili kwa mfano na anaonyesha ya kwamba Kristo ndiye Kichwa mbinguni anayeongoza na kutawala mwili Wake hapa duniani. Ni Kichwa aliye na uwezo na amri, na anayejua maneno na anayeongoza mwili mzima. Uzima mmoja ni kichwani na katika mwili, na vivyo hivyo Kristo hatimii bila Kanisa Lake. Hivi tunasoma katika Waefeso 1:23 ya kwamba Kanisa, mwili Wake, ni "utimilifu wake anayetimiza

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

vyote katika vyote." Neno hili linatushangaza sisi waamini sana na kujaza roho zetu na kuabudu.

**C. WAAMINI WOTE NI VIUNGO KATIKA MWILI WA KRISTO** (Matendo 2:47).

Mara moja wakati mtu anapookolewa, anageuka sehemu ya Kanisa, na kiungo katika mwili wa Kristo, si neno kama ni mtu wa kabila gani, mume au mke, tajiri au masikini, mjinga au mwenye akili, kijana au mzee. Katika 1 Wakorinto 12:12-26 Paulo anatukumbusha ya kwamba:

1. Kuna viungo vingi katika mwili (mash. 12-14).
2. Kila kiungo kina kazi yake kufanya (mash. 15-17).
3. Viungo vina kazi mbalimbali (sh. 19).
4. Kwa mwili kuweza kuwa na afya njema, sharti viungo vyote vitumike pamoja na kila kiungo kitimize kazi yake (mash. 21-23).
5. Kwa sababu viungo vyote vya mwili vinahitajiana, hakuna nafasi kwa hasidi au roho ya uchungu (mash. 15-17) wala kwa majivuno na roho ya kufanya kitu pasipo ushirika wa wengine (sh. 21).
6. Kwa sababu wote ni viungo vya mwili mmoja, inapasa visaidiane na kufarijiana na kufurahi pamoja (mash. 23-26).

**D. ROHO MTAKATIFU NI KATIKA KANISA KWA MAHALI PA KRISTO** ( Yoane 14:16,26) .

Wakati Bwana Yesu alipokwenda mbinguni, alituma Roho Mtakatifu kumkomboa hapa duniani. Tuone maneno mengine Roho Mtakatifu anayofanya katika Kanisa:

1. Anaongoza Wakristo katika kuabudu kwao (Waefeso 2:18).
2. Anasaidia maombi yao (Waroma 8:26,27).
3. Anawapa uwezo wakati wa kuhubiri (1 Watesalonika 1:5).
4. Anawaonyesha nini ambayo inawapasa kufanya (Matendo 13:2), na kuwakataza kufanya maneno mengine yasiyofaa (Matendo 16:6,7).
5. Anachagua wasimamishi kwa Kanisa (Matendo 20:28).

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

6. Anawapa waamini zawadi mbalimbali kwa kusaidia kazi ya Kanisa ili Kanisa liongezeke na kusimama nguvu (Waefeso 4:11).
7. Anaongoza waamini katika kweli yote (Yoane 16:13).

**E. KANISA LA MUNGU NI TAKATIFU** (1 Wakorinto 3:17).

Mungu anaita katikati ya mataifa watu kuwa watu Wake. Anawaweka mbali na dunia ya zambi na anataka watembee kwa utakatifu. Kwa njia ile tu Kanisa linaweza kuonyesha Mungu mtakatifu kwa dunia hii ya zambi.

**F. KRISTO ANALETA ZAWADI MBALIMBALI KWA WATU MBALIMBALI KWA KUJENGA KANISA** (Waefeso 4:11,12).

Ni mapenzi ya Mungu kwa Kanisa kuongezeka kwa imani na kwa ukubwa, ndiyo hesabu ya watu katika Kanisa liongezeke. Na kusudi hili Kristo nyuma ya ufufuko Wake, anatoa zawadi kwa Kanisa. Zawadi hizi ni watu wanaopewa uwezo kuliko wengine kujenga Kanisa. Katika Waefeso 4:11 tunaona wao ni

1. mitume
2. manabii
3. wahubiri wa Habari Njema
4. wachungaji
5. walimu

Tunafikiri kazi ya mitume na manabii ilikuwa zaidi wakati wa mwanzo wa Kanisa (Waefeso 2:20). Hawahitajiwi tena wakati msingi wa Kanisa linapokwisha kuwekwa, na sasa hawana kazi na hawako tena.

Lakini hata sasa tuna wahubiri wa Habari Njema, wachungaji na walimu. Wahubiri wa Habari Njema wanakwenda kwa dunia nzima na Habari Njema, wanaleta wapotevu kwa Kristo, na kisha wanawaongoza kushiriki na kanisa la pahali pale. Wachungaji wanachunga kundi la Mungu, ndio Wakristo, wakiwakulisha na Neno la Mungu na kuwatia roho nguvu, na kuwalinda ubaya usiwapate. Walimu wanaeleza Neno la Mungu hata watu waweze kulifahamu na kujua kweli zote za Mungu.

Wakati watu hawa wanapofanya kazi yao, Kanisa linaende-

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

lea, na watakatifu wanapatishwa nguvu katika imani yao. Mungu analeta zawadi hizi ili Kanisa liongezeke.

**G. WAAMINI WOTE NI MAKUHANI WA MUNGU** (1 Petro 2:5,9).

Katika Agano la Kale watu fulani tu waliweza kuwa makuhani – kabila la Lawi na jamaa ya Haruni (Kutoka 28:1). Sasa watoto wote wa Mungu ni makuhani na wote wanapata faida ya kazi hii na wote wanabeba usimamizi wake.

## 4. Kutimia na mwisho wa Kanisa

Tunakwisha kuona ya kwamba Kanisa lingali linajengwa hata sasa. Halijakwisha bado. Kila mara mtu anapoamini, jiwe hai moja linaongezwa juu ya jengo hili la Mungu. Polepole na pasipo kelele jengo hili linajengwa. Roho Mtakatifu anaongeza kila siku watu wengine wanaookolewa (Matendo 2:47).

Siku moja, nyuma kidogo, kazi hii itakwisha. Jiwe la mwisho litakuwa limewekwa pahali pake na Bwana Yesu atashuka katika mawingu. Kanisa zima litapanda kukutana na Mwokozi, na pamoja watarudi kwa makao mengi yanayongojea Wakristo nyumbani mwa Baba. “Na hivi tutakuwa pamoja na Bwana milele “ (1 Watesalonika 4:17).

Kanisa litakuwa pamoja na Kristo kwa milele, na zaidi ya ile litashiriki katika utukufu alio nao tangu mwanzo (Yoane 17:22).

Halafu kwa milele Kanisa litashuhudia utukufu wa Mungu. “Hata katika nyakati za kuja aonyeshe wingi wa kupita kiasi wa neema yake kwa wema wake kwetu katika Kristo Yesu” (Waefeso 2:7).

Kwa wakati wa sasa Kanisa ni kama mfano kuonyesha kwa falme na mamlaka na watawala wa ulimwengu huu akili kubwa ya Mungu. Hivi inapasa maneno ya Kanisa kuwa kitu kikubwa sana katika roho na mafikiri ya kila mwamini, na inampasa kutumika sana ili Kanisa lijengwe na kuongezeka.

copyright © 1956 William MacDonald All Rights Reserved

# KANISA LA PAHALI FULANI

Tumekwisha kupasha juu ya Kanisa zima lisiloonekana kwa macho, lililo mwili wa Kristo, ndilo waamini wote pahali pote.

Halafu Agano Jipya linafundisha juu ya makanisa kwa pahali fulani vilevile. Kanisa hili ndilo waamini wote wa pahali pale. Hivi tunasoma juu ya makanisa katika Yerusalema, Korinto, Roma, vivyo hivyo. Makanisa haya ni sehemu za Kanisa zima, Kanisa *universel*, lakini kila kanisa linasimama peke yake pahali pake. Makanisa yana ushirika katikati yao, lakini kila kanisa linasimama peke yake mbele ya Kristo na kupata sifa au hukumu Kwake.

Tangu mwanzo wa Kanisa watu wanakwisha kuwa na mafikiri mbalimbali kama Kanisa ni nini. Katika mwaka 1593 Henri Barrow alieleza neno lenyewe hivi: "Kanisa la kweli la Kristo ni waamini wanaofungana pamoja, mbali na wasioamini, na wanaokunsanyika kwa jina la Kristo kwa kumwabudu kweli na kumtii na roho tayari. Wao ni ndugu, ushirika wa watakatifu, na kila mtu ni huru kufanya kitu cho chote ambacho Mungu anamwagiza na kufunua katika Neno Lake takatifu."

Watu wengine walitoa tena mafikiri mengine. Basi tuulize: Agano Jipya linataja maneno fulani yanayohitajiwa ili waamini wa pahali fulani waweze kuhesabiwa kwamba kanisa? Tunafikiri sivyo. Kama waamini wa pahali fulani wakihitaji kutimiza tu utaratibu fulani, ili wahesabiwe kuwa kanisa, neno lenyewe si kitu cha uzima, ni kitu cha desturi tu. Watu watalala tu na kujivuna. Hata kama mara nyingine kanisa linaweza kuonekana vizuri sana, labda hali ya waamini ndani yake si vizuri hata kidogo.

Tunaamini Agano Jipya linatufundisha hivi: Waamini wote, kwa neema ya Mungu, ni sehemu ya Kanisa. Wanafundishwa

kuonyesha kwa namna wanavyokutana pamoja kweli kubwa za Kanisa. Makanisa mengine si mfano mzuri wa mwili wa Kristo. Makanisa mengine ni mfano mzuri kupita. Hakuna kanisa hata moja linalotimia.

Hivi tusiseme: "Kama mukifanya hivi na hivi mutakuwa kanisa." Mafundisho ya Maandiko Matakatifu ni mafundisho ya neema na yanasema hivi: "Ninyi ni waamini na muko kanisa. Basi sasa kwa namna munavyokutana mwonyeshe neno hili wazi kwa dunia." Ni mapendo kwa Mwokozi ambayo yanatusukuma na kutupa kutaka hata kanisa letu liwe mfano mzuri wa mwili wa Kristo kwa wale ambao wanatuzunguka.

Hivi tunaona ya kwamba linapasa kanisa la pahali pamoja kuwa mfano wa Kanisa zima. Haifai lifanye kitu kitakachokana kweli kubwa za Kanisa zima ndilo mwili wa Kristo.

Sharti umoja wa Kanisa uonekane. Sharti watu waweze kuona ya kwamba Kanisa ni mwili wa Kristo na ya kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani yake, na ya kwamba waamini wote ni viungo ndani yake, na wanaunganishwa pamoja na Kristo katika utukufu na wanaunganishwa pamoja katikati yao vilevile. Sharti Kanisa lionyeshe ya kwamba kurudi kwa Kristo ni taraja yake na ya kwamba linaitwa na jina la Kristo tu.

Basi kama kanisa la pahali fulani ni mfano wa kanisa zima, inalipasa kuonyesha maneno gani ili liwe mfano wa mwili wa Kristo? Tulitaja maneno saba mbele, ndiyo haya:

A. Kanisa la Kristo ni mwili mmoja.
B. Kristo ni kichwa cha mwili.
C. Waamini wote ni viungo vya mwili.
D. Roho Mtakatifu ni Mkombozi wa Kristo katika Kanisa.
E. Kanisa la Mungu ni takatifu.
F. Kristo analeta zawadi kwa kujenga Kanisa.
G. Waamini wote ni makuhani kwa Mungu.

Sasa tutajaribu kueleza maneno haya yote moja moja na kuonyesha namna gani kanisa la pahali pamoja linaweza kuyaonyesha kwa dunia.

# KANISA LA KRISTO NI MWILI MMOJA

Namna gani waamini wa pahali pamoja wanaweza kuonyesha neno hili ?

1. Kwa njia ya kukataa kuwa na jina ambalo litawagawa na waamini wengine. Katika kanisa la Korinto wengine walikuwa wakisema, "Mimi ni wa Paulo," "(Mimi ni wa Apolo," au "Mimi ni wa Kristo." Paulo alikataa masemo namna hii kabisa kabisa, akauliza, "Kristo amegawanyika?" (1 Wakorinto 1:10-17).

   Leo Wakristo wengi wanajiita na majina mbalimbali, kama Baptiste, Méthodiste, Pentacostale, na hivi na hivi, kwa sababu utaratibu wao katika kanisa lao ni mbalimbali kidogo na utaratibu wa makanisa mengine. Wengine wanabatiza mtu katika maji, wengine wanamwanga maji nusu juu ya kichwa chake. Wengine wanaacha Wakristo tu kukutana kwa meza ya Bwana, wengine wanaacha watu wengine kufika vilevile. Wengine wanapokea waamini wa kweli tu katika kanisa, wengine wanapokea hata watu wengine vilevile. Kwa njia hizi Wakristo wanagawanyika na wanajiita na majina mbalimbali, na neno lenyewe linakana umoja wa mwili wa Kristo waziwazi.

2. Mungu anataka watoto Wake kujulikana na majina yanayotajwa katika Biblia tu, kama "waamini" (Matendo 5:14), "wanafunzi" (Matendo 9:1), "Wakristo" (Matendo 11:26), "watakatifu" (Waefeso 1:1), na "ndugu" (Yakobo 2:1). Ni nguvu sana kwa Mkristo kukataa majina yote mengine ila majina haya. Zaidi ya Wakristo leo wanafikiri sharti waungane na kanisa kubwa fulani linalojulikana na lililo na jina lisiloonekana ndani ya Agano Jipya. Mtu yule anayekubali kuitwa "mtoto wa Mungu" tu anazarauliwa hata na

Wakristo wengine. Lakini namna gani Mkristo anayetaka kupendeza Bwana yake kweli kweli anaweza kufanya kitu kingine?

3. Lakini haitoshi tu kuwa na jina namna ya majina yanayotajwa katika Biblia. Haifai kujivuna juu ya jina na kufikiri "Mimi tu ninafanya vizuri -- wale wote wengine wanafanya vibaya" kwani neno hili vilevile linakana maneno ya umoja wa mwili wa Kristo. Katika Korinto wengine walikuwa wakisema, "Mimi ni wa Kristo." Walijivuna juu ya jina hili lakini kabisa kabisa walifikiri ya kwamba wao tu walikuwa wa Kristo, si waamini wengine. Paulo aliwahamakia namna alivyohamakia wale waliosema wao ni wa Apolo.
4. Wakati unapojaribu kuonyesha ya kwamba si vizuri kwa makanisa kujiita na majina mbalimbali, wengine wanasema ya kwamba Mungu anakwisha kubariki mengine ya makanisa haya sana. Neno hili ni kweli, lakini tukumbuke ya kuwa:
   a. Hata kama Bwana akibariki, neno hili halionyeshi ya kwamba anakubali kila kitu kinachofanywa. Mungu anaheshimu Neno Lake, hata kama mara nyingi linahubiriwa pamoja na kuanguka sana. Kama Mungu angalibariki tu watu wanaotimia kabisa, baraka itakosa pia. Hivi hata kama Mungu anabariki kazi ya wengine, neno hili halionyeshi ya kwamba anakubali kila kitu wanachofanya. Neno Lake ni kubwa kuliko mhubiri yule ambaye analihubiri.
   b. Ona mafikiri ya Bwana juu ya magawanyiko katika kanisa kwa 1 Wakorinto 3:4, "Kwa sababu wakati mtu mmoja anaposema: Mimi ni wa Paulo, na mwingine, Mimi ni wa Apolo; ninyi si watu wa mwili?"
   c. Magawanyiko katika kanisa yanaleta maneno mabaya mengi.
      1) Yanagawa waamini wasiwe na ushirika katikati yao.
      2) Yanafunga njia ya watumishi wa Mungu wenye zawadi ya kuhubiri kutembea katikati ya Wakristo wote na kufundisha.
      3) Yanaleta shaka kwa dunia na watu wanauliza, "Kanisa la wapi ndilo kanisa la kweli?"

Mungu atusamehe kwa sababu ya magawanyiko. Yanaangusha watu wa dunia sana. Ilipasa watu wa dunia kusema: Ona namna Wakristo wale wanavyopendana!" Lakini mara nyingi wanalazimishwa kusema, "Ona namna wanavyogombana katikati yao na kuhukumana na kusingiziana."

5. Waamini wanaokusudi kushuhudia umoja wa mwili wa Kristo wataona matata sana wakati wanapojaribu kujichunga mbali na magawanyiko yote katika kanisa, na hata hivi kuwa na roho ya mapendo kwa watoto wote wa Mungu. Tunahitaji neema ya Mungu kuweza kuona Kristo ndani ya wengine walio na mafikiri mbali na mafikiri yetu.
6. Hatuwezi kuonyesha umoja wa mwili wa Kristo kwa njia ya comités kubwa za wachaguliwa wa makanisa mbalimbali wanaokutana pamoja. Waamini wa kweli wanakana Bwana yao wakati wanapoungana pamoja na wale wasioamini ya kwamba Kristo alizaliwa na bikira Maria, ya kwamba tunapata ukombozi kwa njia ya kufa Kwake, ya kwamba alifufuliwa na alikwenda mbinguni na atarudi tena.
7. Neno lile linalopasa kufunga Wakristo wote pamoja ni mapendo yao kwa Bwana yao na kwa Neno Lake. Wakati hamu kubwa ya roho zetu ni kumtukuza Yeye tu, tutakuwa na roho moja na halafu maombi ya Bwana Yesu yatapata jibu: *"Wakae mmoja **kama sisi** tulivyo mmoja"* (Yoane 17:22).

Basi kazi kubwa ya kanisa kwa pahali fulani ni kuonyesha umoja wa mwili wa Kristo. Wanaweza kufanya hivi kwa njia ya kukubali waamini wote kama ndugu zao katika Kristo.

# KRISTO NI KICHWA CHA MWILI, NDILO KANISA

Namna gani waamini wanaweza kuonyesha neno hili?

1. Kwa njia ya kukataa kuwa na mtu wa dunia kuongoza.
2. Tunaonyesha wazi ya kwamba Kristo ni Kichwa cha kanisa wakati tunapompa njia kutawala na kuongoza kazi zote za kanisa na kukata maneno yote. Labda watu wanaweza kuuliza, "Neno hili litawezekana namna gani? Namna gani Bwana aliye mbinguni ataweza kuongoza kanisa lililo hapa duniani?" Lakini tunajua kabisa ya kwamba watu wakimngojea na saburi kujua mapenzi Yake, atayafunua kwao. Ndiyo, neno hili linaomba saburi na maombi. Ni nyepesi zaidi kuongoza maneno sisi wenyewe. Lakini tukumbuke ya kwamba tunaweza kutimiza utaratibu wa Agano Jipya kwa njia ya uwezo wa Roho Mtakatifu tu, na wale wasio tayari kumtegemea Yeye na kuomba na kumngojea na saburi hawataona namna gani Kichwa cha Kanisa, ndiye Kristo, anaongoza kanisa la pahali fulani hapa duniani.
3. Tusiseme na kinywa tu ya kwamba Kristo ni Kichwa cha Kanisa na halafu kubisha neno lenyewe na matendo yetu. Kuna wengine wanaosema na nguvu yote ya kwamba Kristo ni Kichwa cha Kanisa, lakini masemo yao ni bule kwani wao wenyewe wanatawala kanisa na nguvu. Wanajifanyiza kuwa kama wafalme katika kanisa. Diotrefe alikuwa mtu wa namna hii (3 Yoane 9,10). Alitaka sana kuwa mtu wa kwanza. Alisema maneno mabaya juu ya watu wa Mungu kama Yoane na alikataa kuwapokea. Alikataza hata watu wengine kuwapokea, na kama waliwapokea hata hivi, aliwafukuza toka kanisa. Neno namna hii linakana ya kwamba Kristo ni Kichwa cha Kanisa.

# WAAMINI WOTE NI VIUNGO VYA MWILI MMOJA

## Maneno ya kupokea katika kanisa

Inapasa kanisa kupokea wanani?

1. Inapasa kanisa kupokea wote wanaokwisha kupokewa na Kristo. "Kwa hii mukaribishane, kama Kristo alivyotukaribisha kwa utukufu wa Mungu" (Waroma 15:7).
2. Lakini kuna maneno mengine kukumbuka vilevile:
    a. Sharti mtu huyu awe na ushuhuda mzuri (1 Wakorinto 5:11; 10:21). Si mfano mzuri wa utakatifu wa kanisa kupokea mzini, au mwenye tamaa, au mwenye kuabudu sanamu, au mtukanayi, au mlevi, au mnyanganyi.
    b. Haifai kupokea mtu anayeondoshwa katika kanisa lake la mbele kwa sababu ya zambi aliyofanya (1 Wakorinto 5:13). Kupokea mtu wa namna hii ni kukana umoja wa mwili wa Kristo (Waefeso 4:4). Kufika wakati mtu huyu anapotengeneza maneno yake na ana upatano mzuri na Bwana na watu Wake tena, inapasa kumhesabu kama mtu wa mataifa au mtoza kodi (Matayo 18:17).
    c. Sharti mtu anayetaka kupokewa ajue na kukubali mafundisho ya Kristo (2 Yoane 10). "Mtu akikuja kwenu, naye haleti mafundisho haya, musimkaribishe nyumbani mwenu, wala musimpe salamu." Halafu mafundisho ya Kristo ni nini? Ya kwamba Yeye ni Mungu, alizaliwa na bikira, hakufanya zambi, alikufa kwa pahali petu kutuokoa, alizikwa, alifufuliwa, alikwenda mbinguni na atarudi tena.

Basi kujumlisha maneno haya yote, inapasa kanisa kupokea waamini wote wa kweli walio na mwenendo safi na wasioondoshwa katika kanisa lingine kwa sababu ya zambi waliyofanya, na wanaosimamia mafundisho ya Kristo.

3. Lakini Maandiko Matakatifu yana maagizo mengine vilevile juu ya maneno ya kupokea. Inapasa kanisa kupokea:
    a. Mtu aliye zaifu kwa imani (Waroma 14:1). Hapa Paulo anasema juu ya mwamini anayeangalia mwenendo wake sana kwa maneno mengine yaliyo maneno bule bule. Kwa mfano, kama mtu akikataa kula nyama kwa sababu anafikiri kula nyama ni zambi, inapasa kumpokea hata hivi.
    b. Tusiwe na upendeleo kwa maneno ya kupokea watu (Yakobo 2:1-5). Tusibembeleze watajiri na kuzarau wamasikini. Tusiweke tofauti katikati ya makabila vile vile. Tofauti haifai kwa Mkristo.
    c. Inapasa kupokea mwamini wa kweli hata kama hajui maneno mengi (Matendo 9:26-28). Kitu kikubwa si kama anakwisha kujua ngapi, lakini kama anajua Kristo. Hivi Apolo alipokewa kwa Efeso hata kama kwa maneno mengine alikuwa mjinga (Matendo 18:24-28).
    d. Haifai kukataa mwamini wa kweli kwa sababu hajabatizwa bado. Ndiyo, inapasa waamini wote kubatizwa (Matayo 28:19), lakini hatuwezi kusema ya kwamba hatuwezi kupokea mtu fulani kwa sababu hajabatizwa bado.
    e. Wakati wa kupokea mtu, haifai kukumbuka kama mtu yule alikuwa mtu wa namna gani mbele ya kuokolewa. Paulo alikuwa mtesaji mbele, lakini alipokewa hata hivi (Matendo 9:27,28); Onesimo alikuwa mwizi mbele, lakini Paulo alionya Filemono kumpokea (Filemono 12,15).
    f. Inatupasa kupokea waamini wa kweli na furaha (Wafilipi 2:29). Namna tunavyotendea Mkristo aliye zaifu sana, namna hii tunatendea Kristo Yeye Mwenyewe. “Kwa kadiri mulivyotendea mmoja wa ndugu zangu, walio wadogo, mulinitendea mimi” (Matayo 25:40).
4. Halafu tunaweza kuuliza neno lingine: Namna gani kanisa litaweza kujua kama mtu aliokolewa kweli kweli na inafaa kumpokea katika kanisa? Tunaweza kutaja njia tano zinazosaidia.

a. Barua ya kanisa pahali alipotoka (Waroma 16:1). Inasaidia Mkristo anayesafiri kuwa na barua ya kanisa lake kuonyesha ya kwamba yeye ni mwamini wa kweli na mwenendo wake ni safi.

b. Ushuhuda wa washuhuda wawili au watatu (Matayo 18:16). Kama Wakristo wawili au watatu katika kanisa wakijua mtu huyu ni mwamini wa kweli na mwenendo wake ni mzuri, kanisa linaweza kumpokea.

c. Ushuhuda wa mtu mmoja tu kama kanisa linakubali neno mtu huyu analosema kwa sababu wanamwamini kuwa mtu wa haki. Paulo alisema na Wakristo wa Roma kupokea Foibe (Waroma 16:1), na alisema na Wakristo wa Filipi kupokea Epafrodito (Wafilipi 2:28-30).

d. Kama mtu akijulikana kama mtumishi wa Kristo (2 Wakorinto 3:1-3) inapasa kanisa kumpokea. Paulo alikataa kuwa na barua kwa kuonyesha kanisa la Korinto kwa sababu walijua vizuri ya kwamba yeye ni mtume wa Yesu Kristo.

e. Wazee wanaweza kuulizana na mtu huyu wao wenyewe kuona kama yeye ni mwamini wa kweli.

5. Halafu mbele ya kumaliza sura hii, kuna maneno matatu mengine watu wanayouliza:

   a. Kanisa lina ruhusa kweli kusema fulani ameokolewa ama sivyo?

      Ndiyo, sharti kanisa litafute neno hili. Wakristo wanakatazwa kuwa na ushirika pamoja na wasioamini (2 Wakorinto 6:14,17). Hivi ni sharti kwao kujaribu kwa njia yo yote wanayoweza kufahamu kama fulani ni mtu wa Mungu kweli ama sivyo, mbele ya kumpokea katikati yao.

   b. Inapasa kufanya nini wakati mtu anayekwisha kupokewa na kanisa anaposimama na kufundisha maneno yasiyo sawa?

      Inapasa kubisha mafundisho yake waziwazi mbele ya watu wote kwa njia ya Neno la Mungu. Ni kazi ya wazee

kuonyesha ubaya wa mafundisho yake na kusimamia imani (Tito 1:9).

c. Halafu kanisa litafanya nini kama nyuma ya kupokea mtu fulani, mtu huyu hakutani mara zote na ndugu za kanisa lakini anafika wakati mmoja mmoja tu, au labda anaacha kufika mara moja?

   Kama akifika wakati mmoja mmoja tu, inapasa kumfundisha ya kwamba ushirika katika kanisa ni ushirika katika kazi ya kanisa na responsabilité vilevile. Inapasa kila mtu katika kanisa kubeba sehemu yake ya kazi ya kanisa. Mtu anayefika mara moja tu kila juma si katika ushirika wa kanisa lile kweli.

   Kama mtu yule aliyepokewa hafiki tena, ni neno lake mbele ya Mungu. Kanisa halina hukumu ndani yake.

# ROHO MTAKATIFU KATIKA KANISA

Kitu kikubwa ambacho inatupasa kufahamu ni ya kwamba Roho Mtakatifu ndiye mjumbe wa Kristo katika Kanisa.

Wakati utakapofikiri juu ya neno hili kwanza, labda utasema neno hili halipatani na maneno tunayokwisha kusema ya kwamba Kristo ni Kichwa cha Kanisa. Lakini maneno yale yote mawili ni kweli. Kristo ni Kichwa na ameweka Roho Mtakatifu kuwa mjumbe Wake hapa duniani. Hivi ni sharti kwa kila kanisa kumpa Roho Mtakatifu ya Mungu pahali pake pa heshima.

Tutafanya hivi namna gani?

1. **Kwanza, inapasa kanisa kuomba Roho Mtakatifu kuwaongoza katika maneno yote, kama**
   a. kuchagua pahali pa kukutana pamoja
   b. utaratibu wa makusanyiko
   c. kuchagua wahubiri watakaohubiri Neno la Mungu
   d. kutumika na mali ya kanisa
   e. kuhukumu maneno ya zambi yanayotokea katika kanisa.

2. **Neno la pili, inapasa kukumbuka ya kwamba Roho Mtakatifu ana ruhusa yote.** Anaweza kufanya kitu cho chote anachotaka na mara nyingine anaongoza Wakristo wa kanisa moja kufanya maneno yao namna nyingine na Wakristo wa kanisa lingine. Lakini maneno yote anayoongoza Wakristo kufanya yanapatana na mafundisho ya Neno la Mungu.

   Makanisa ya mwanzo yalikuwa hivi. Roho Mtakatifu aliongoza watu wote. Wakati Roho Mtakatifu aliposhukia Kanisa wakati wa Pentekote alikaa juu yao kwa mfano wa ndimi za moto. Midomo yao ikafunguliwa na kila mtu ali-

tangaza kazi kubwa za Mungu. Watu waliopata wokovu waliwaka kwa Roho Mtakatifu. Wakati walipozaliwa tena, walizaliwa tena kweli kweli. Maisha yao yaligeuka kabisa, walipata uwezo mpya, hamu kubwa kwa kutembea kwa utakatifu, ufahamu kwa Maandiko Matakatifu, na mara nyingine walipata uwezo mpya kwa kuhubiri. Katika 1 Wakorinto Paulo anatuonyesha namna gani kanisa moja kwa wakati wa mwanzo lilivyokuwa. Hakuna mtu katikati yao aliyenyamaza. Wakati walipokutana pamoja, kila mtu alikuwa na zaburi, na ufunuo, na unabii, na tafsiri. Roho Mtakatifu aliwaka ndani yao yote. Wakati watu walipookolewa wakati ule, neno lenyewe liligeuza maisha yao kabisa kabisa.

Lakini neno hili lilikuwa na matata yake vilevile. Hata kama Mkristo alikuwa amepokea Roho Mtakatifu, yeye alikuwa mtu tu na mara nyingine furaha yake mpya na hamu yake kufanya kitu kwa Mungu zilimsukuma kufanya maneno yasiyokuwa taratibu kabisa. Mara nyingine aliweza kufungua kinywa chake (kwani katika kanisa la mwanzo kila mwanamume alikuwa na ruhusa kusema) wakati ingalipokuwa vizuri zaidi kunyamaza. Au labda namna mwamini mpya alivyojaribu kuhubiri haikuweza kufurahisha wazee. Na kwa njia hii wazee wakaanza kupima kufunga njia ya vijana, na kwa njia hii kuzima moto wa Roho Mtakatifu ndani yao. Kuhamakia Mkristo mwingine bila mapendo, kunyamaza kimya wakati inapopasa kusemezana naye, kumwona bule, maneno haya yote yanazima uwezo na moto wa Roho Mtakatifu.

Hivi kwa sababu watu walijaribu kuchunga utaratibu wa kanisa, Roho Mtakatifu hakuwa na uwezo kuongoza watu wa Mungu tena. Wengine wa Wakristo walianza kusimama kama watawala na polepole wao tu walikuwa na ruhusa kuhubiri na kuomba na kuongoza kanisa la Mungu. Ilikuwa kama kwa njia yao tu watu waliweza kufika karibu na Mungu. Watu wengine katika kanisa hawakuwa na ruhusa tena kushiriki katika kazi ya kuhubiri na kuomba. Hivi Roho Mtakatifu alizimwa wakati Wakristo walipokutana pamoja kwa kuabudu.

Katika makanisa mengine neno lenyewe ni hivi hata wakati wa sasa. Lakini makanisa mengine walitomboka, wakapima kurudisha utaratibu wa zamani tena, na katikati yao kila mwanamume ana ruhusa kufundisha na kuhubiri na kuomba namna Roho Mtakatifu anavyomwongoza.

3. **Haifai kufunga njia ya Roho Mtakatifu kuongoza kwa njia ya kuweka maagizo mbalimbali.** Haifai kusema kusanyiko sharti likwishe saa fulani. Si sharti kwa kusanyiko kuwa sawasawa kila mara, kwa mfano: Kwanza watu wataimba nyimbo mbili, kisha mtu mmoja ataomba na halafu mtu mwingine atahubiri. Halafu mtu wa kwanza ataomba tena na watu wataimba wimbo mmoja, kisha watatoka. Labda mara nyingine Roho Mtakatifu anataka Wakristo kuimba nyimbo tatu kwa mwanzo. Labda wakati mhubiri wa kwanza anapomaliza na Wakristo wanapokwisha kuimba wimbo, Roho Mtakatifu anataka kuongoza ndugu mwingine kuongeza mafundisho mengine. Vivyo hivyo.

Kama katika makanisa yetu Roho Mtakatifu ni huru kuongoza Wakristo kweli kweli, na kama Wakristo wakitii kuongoza Kwake, makanisa yetu yatawaka kwa moto wa Roho Mtakatifu, na wasioamini wataokolewa, na Wakristo watatembea kwa haki.

# KUHUKUMU ZAMBI KATIKA KANISA

Kwa kanisa la pahali fulani kuwa mfano wa Kanisa la Mungu, **sharti kanisa hili liwe takatifu.**

Neno hili litawezekana namna gani?

1. Inapasa watu wote wa kanisa kutembea kwa utakatifu. Mungu anataka tutakaswe kwa mwenendo wetu (1 Watesalonika 4:3). Maana ya Kanisa haiko utaratibu fulani wa kuabudu tu, lakini inapasa Wakristo washuhudie kweli ya Mungu kwa njia ya mwenendo wao vilevile. Kwa hivi mafundisho juu ya utaratibu wa kanisa unachanganyana na mafundisho kwa mwenendo wa Wakristo pahali pote katika Agano Jipya.
2. **Kwa kusaidia neno hili, sharti Wakristo wapate mafundisho ya kuwafaa katika Kitabu cha Mungu.** Haifai tu kwa mhubiri kuchagua mashairi fulani siku moja na tena mhubiri mwingine kuchagua mashairi mengine katika kitabu kingine cha Biblia siku nyingine. Sivyo. Sharti mafundisho yafuatane kusudi Wakristo wapate mafundisho juu ya kitabu kimoja kizima, juu ya maisha mazima ya watu wa Biblia kama Daudi, Elia, Noa, Abrahamu, vivyo hivyo. Sharti wapate mafundisho juu ya kweli mbalimbali za Mungu kama usamehe wa zambi, kurudi kwa Kristo, kazi ya Roho Mtakatifu, maombi, vivyo hivyo. Kwa njia ile tu Wakristo watapokea Neno zima la Mungu.
3. Hata kama mafundisho ya Neno la Mungu yanapunguza maneno ya zambi katika kanisa, **inapasa Wakristo kuhukumu zambi mara nyingine katikati yao hata hivi.** Wakati mtu mmoja anapoanguka kwa zambi, zambi hii inafanyiza kanisa zima kuwa zaifu, na inaharibu ushuhuda wake mbele ya watu wa dunia. Hivi sharti zambi hii ihukumiwe. “Kwa maana wakati umefika kwa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu” (1 Petro 4:17).

4 **Kuhukumu zambi katika kanisa kuna faida kwa njia mbili:**

a. Kwanza, ni kuonyesha wazi ya kwamba mtu fulani anayesema yeye ni Mkristo, hakuamini kweli, na kumwondosha katika kanisa. Tunasoma juu ya watu namna hii katika 1 Yoane 2:19.

b. Kuazibu mwamini aliyeanguka hata aweze kurudi karibu na Bwana na kwa kanisa. Wakati Mkristo anapopata azabu, si kwa sababu ya kumlipiza tu kwa ubaya aliofanya lakini zaidi ni hata azabu hii iweze kumrudisha karibu na Bwana.

5. **Katika Agano Jipya tunaona njia mbalimbali kwa kuazibu na kuhukumu Wakristo.** Tutataja njia nyingine.

a. Kama ndugu mmoja akikosea ndugu mwingine, inapasa kusemezana na yule aliyekosa kwanza peke yake. Kama akikataa kusikia, halafu mtu mmoja au watu wawili wengine waende karibu naye. Kama hasikii maonyo yao vilevile, inapasa kumleta mbele ya kanisa. Na kama hata neno hili halimsaidii, inapasa kumhesabu kama mtaifa na mtoza kodi (Matayo 18:15-17), maana yake kuacha kuwa na ushirika naye.

b. Njia nyingine ni **maonyo** (1 Watesalonika 5:14). Inapasa kutumika na njia hii wakati Mkristo fulani asipokaa na utaratibu, maana yake anakataa kutii na kunyenyekea wale walio juu yake katika Bwana.

c. Tena tunasoma juu ya watu namna mbili ambao inatupasa kuepuka nao. Ni watu wasiotembea na utaratibu (2 Watesalonika 3:11,14,15), na wale wanaoleta magawanyiko katikati ya watu wa Mungu (Waroma 16:17). Mtu asiyetembea na utaratibu ni mtu anayekataa kufanya kazi. Tena mtu yule anayeleta magawanyiko katikati ya watu wa Mungu anafanya hivi hata watu waweze kumfuata yeye, yeye mwenyewe apate faida na heshima.

d. Mtu mzushi, maana mtu anayefundisha maneno yasiyopatana na Kitabu cha Mungu, inapasa kumkataa kama akikataa kusikia maonyo mara ya kwanza na mara ya pili (Tito 3:10). Si wazi kabisa kama maana ya kukataa hapa ni

kumwondosha katika kanisa au kama ni azabu ya namna nyingine.

e. Tena azabu kubwa zaidi ni kuondosha mtu katika kanisa (1 Wakorinto 5:11,13). Azabu hii ni kwa wale wanaotenda uasherati, wenye tamaa, watu wanaoabudu sanamu, watukanayi, walevi na wanyanganyi.

6. Wakati wa kufikiri maneno ya kuhukumu na kuazibu katika kanisa, **inatupasa kukumbuka ya kwamba haifai kukata kitu pasipo kuwa na washuhuda**. Sharti washuhuda wawe wawili au watatu au zaidi. Hata kama unafikiri fulani ni mtu wa haki kabisa na hawezi kusema uwongo, agizo la Mungu ni washuhuda wawe kuliko mmoja. "Kwa vinywa vya washuhuda wawili au watatu kila neno lisimamishwe" (Matayo 18:16).

   Basi utafanya nini kama wewe peke yako ukijua zambi fulani ya ndugu mmoja au ndugu wengine? Utaomba Mungu kusimamisha washuhuda wengine. Haifai kuonyesha zambi ile wazi wakati wewe ni mshuhuda wa pekee. Na usifazaike na kuumizwa katika roho kama watu wasipopokea ushuhuda wako kama wewe ni mshuhuda wa pekee. Ni agizo la Mungu washuhuda wawe wawili au zaidi.

7. **Maneno mengine ambayo inatupasa kukumbuka wakati tunapolazimishwa kuazibu ndugu mmoja ya kanisa:**

   a. Sharti tufanye neno lenyewe na roho ya unyenyekevu tukijiangalia nafsi zetu tusijaribiwe sisi wenyewe (Wagalatia 6:1).

   b. Sharti hukumu iwe pasipo upendeleo. Hata kama yule aliyefanya zambi hii ni ndugu yetu au rafiki ya karibu, inapasa kumhukumu kama mtu mwingine, pasipo upendeleo (Torati 1:17; Yakobo 2:1).

   c. Kama inapasa kuondosha Mkristo mmoja toka kanisa, hii ni kazi ya kanisa zima, si ya mtu mmoja tu (2 Wakorinto 2:6). Ni neno la huzuni sana wakati inapotupasa kuondosha ndugu mmoja toka kanisa. Haifai tu kusema kwa mwisho wa kusanyiko moja la kanisa ya kwamba mtu fulani anakwisha kuondoshwa toka kanisa. Hapana. Inapasa kanisa zima kukutana pamoja kwa neno lile lile tu, pamoja

na huzuni na machozi. Si kazi ya kanisa zima kukata neno lenyewe. Hii ni kazi ya wazee. Halafu wakati wao wanapokwisha kukata neno lenyewe, inapasa kanisa zima kukutana na kuondosha mtu yule katikati yao na huzuni na unyenyekevu, kila mtu akijihukumu mwenyewe na kutafuta roho yake mbele ya Mungu vilevile.

8. Tena tukumbuke ya kwamba **haifai kwa Wakristo kutangaza zambi za ndugu zao pahali pote,** lakini kuficha neno lenyewe mbele ya wasioamini (Mwanzo 9:23).

Kama ndugu za kanisa wasipohukumu watenda zambi katikati yao, kanisa lile halitakuwa mfano mzuri wa hekalu takatifu la Mungu.

Tukumbuke vilevile ya kwamba katika Agano Jipya kila Mkristo ni mtu wa kanisa fulani moja. Kama asipokuwa katika kanisa fulani, hakuna kanisa litakaloweza kumhukumu wakati anapoanguka, na neno hili ni hatari kubwa sana kwake.

# KUONGEZEKA KWA KANISA

## Zawadi kwa kujenga kanisa

1. Wakati Wakristo wanapojengwa katika imani, kanisa linaongezeka. Hili ndilo neno Mungu analotaka sana. Inapasa Wakristo wa kila kanisa kutafuta njia wakati wote namna gani wataweza kuongeza kazi yao kugusa tena watu wengine na wengine na Habari Njema hata makanisa mengine mapya yasimamishwe.

   Kama tulivyoonyesha mbele, Kristo, Kichwa cha Kanisa, anakwisha kuleta zawadi kwa Kanisa, na kama Wakristo waliopewa zawadi hizi wakitumika nazo, namna inavyofaa, kanisa linaongezeka.

2. Tulisema mbele ya kwamba kwa mwanzo zawadi zilikuwa tano: Mitume, manabii, wahubiri wa Habari Njema, wachungaji, na walimu. Ni kama zawadi mbili za kwanza zilitumika zaidi kwa wakati wa mwanzo wa kanisa, na ya kama hazikuhitajiwa tena wakati watu walipokwisha kupata Biblia nzima mikononi mwao. Halafu tunabaki na zawadi tatu wakati wa sasa: wahubiri wa Habari Njema, waangalizi na walimu. Tuone sasa kwa nini zawadi hizi zililetwa na namna gani zinatumika wakati wa sasa.

3. Tunaona kwa nini Kristo alileta zawadi hizi katika Waefeso 4:12,13, "Kwa kusudi la kukamilisha watakatifu, kwa kazi ya utumishi, hata mwili wa Kristo ujengwe, hata sisi sote tufikie umoja wa imani, na kujua sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mzima, hata kufika kipimo cha urefu wa utimilifu wa Kristo." Hivi tunaona zawadi hizi zinaletwa ili Wakristo wakamilishwe na halafu waweze kuwa tayari kwa utumishi wa Kristo hata mwili wa Kristo, ndio Kanisa, upate kujengwa.

Kwa mfano mwalimu mmoja anafundisha watu wane na kuwatayarisha hata wao tena waweze kufundisha watu wengine. Halafu kila mmoja katikati yao anafundisha tena watu wane wengine na kuwatayarisha kwa kazi ya Bwana vilevile. Sasa hesabu ya wale wanaofundisha wengine inakwisha kuongezaka kabisa. Kwa pahali pa mwalimu mmoja sasa kuna ndugu 16 wanaofundisha kila mtu watu wane wengine.

Kazi ya wahubiri wa Habari Njema na wachungaji na walimu ni kila mara kutayarisha watu wengine kwa kazi ya Mungu.

Hata kama si kila mtu aliye na moja ya zawadi hizi, inapasa kila Mkristo kushiriki katika kazi ya Mungu. Inapasa kila mtu ndani ya kanisa kuwa mtu wa kuabudu, mtu wa kutafuta watu wengine kwa Kristo, mtu anayetafuta na kujifunza Neno la Mungu yeye mwenyewe, mtu anayeendelesha kazi ya Mungu mbele.

Tunaona maneno haya katika 2 Timoteo 2:2 vilevile, "Na maneno yale uliyosikia kwangu kwa washuhuda wengi, maneno haya uwekee watu waaminifu watakaofaa kufundisha wengine vile."

4. Maneno haya yana faida nyingi. Yanaendelesha mafundisho ya Kristo katikati ya watu mbio. Tena yanasaidia vilevile Wakristo wale wanaojaribu kufanya kazi hii kwani kwa njia ya kuifanya watapata nguvu wao wenyewe katika imani, na hawataangushwa mbio na mafundisho ya uwongo.
5. Halafu tufikiri kwanza maneno yanayoonekana pahali pingi katikati ya watu wa Mungu. Mtu mmoja anachaguliwa kuwa pasteur ya kanisa. Ni yeye anayehubiri, na kubatiza watu na kuongoza kuabudu kwa meza ya Bwana na kufanya maneno yote mengine katika kanisa. Watu wanasikiliza mafundisho yake kila juma, lakini wingi katikati yao hawako tayari kusaidia na kazi ya kanisa wao wenyewe, Wanafikiri wanalipa pasteur salaire, basi hivi yeye afanye. Hivi wanasikiliza mafundisho ya watu wengine tu na hawajuani na Neno la Mungu wao wenyewe zaidi. Wanabaki kama watoto na wanatupwa huko na huko na kuchukuliwa

kwa kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu kwa ujanja, kwa udanganyifu mbaya (Waefeso 4:14).

Halafu kwa pasteur huyu ni ngumu kufanya kazi hizi nyingi, kwani yeye ni mtu mmoja tu. Lakini kama watu wale wote wangalitumikia Bwana pamoja na roho moja, kama kazi nyingi zaidi ingalifanyika.

6. Halafu tunaweza kuuliza: Kwa kanisa kuongozwa na pasteur mmoja tu anayefanya kazi zote ni sawasawa na agizo la Biblia?

   Kwanza tunataka kusema ya kwamba wingi wa watu wanaokwisha kufanya kazi ya pasteur ya kanisa fulani walikuwa watu wa Mungu kabisa na Mungu alitumika sana nao kuokoa watu wengi. Wengine katikati yao wanakwisha kuandika vitabu vizuri sana kueleza maana ya Maandiko Matakatifu na tunashukuru Mungu kwa sababu yao.

   Hata hivi wakati tunapoangalia ndani ya Agano Jipya, hatuoni wapasteur namna hii pale. Hatuoni pahali po pote mtu mmoja tu akiongoza kanisa. Tunafikiri maneno yale yanakana mafundisho ya Agano Jipya.

   a. Kwanza, Agano Jipya linatufundisha ya kwamba waamini wote ni makuhani mbele ya Mungu (1 Petro 2:5,9). Kwa wakati wa Agano la Kale makuhani tu, ndio wana wa Haruni, waliweza kusimama mbele ya Mungu na kutoa sadaka kwa ajili ya watu. Walikuwa kama wapatanishi katikati ya Mungu na watu. Lakini wakati wa sasa waamini wote ni makuhani, wao wote wanaweza kukaribia Mungu na sadaka zao za sifa na kuabudu. Lakini wakati kuna mtu mmoja tu anayeongoza maneno yote katika kanisa, vinywa vya watu wote wengine vinafungwa na hawatoi sifa kwa Mungu kama inavyowapasa kufanya.

   b. Kuwa na pasteur mmoja tu kwa kanisa moja kunazuiza watu wasitumike na zawadi ambazo Mungu aliwapa kwa kumtumikia nazo katika kanisa (1 Wakorinto 12 na 14). Ni mtu yule mmoja tu aliye na ruhusa kufanya kazi hizi wao wote wanazopaswa kushiriki ndani yao.

   c. Tena pasteur mmoja tu akiongoza kanisa, yeye tu ana

ruhusa kuvunja mkate kwa meza ya Bwana na kuwapa watu mvinyo kwa ukumbusho wa mauti ya Kristo. Hatuoni neno hili katika Agano Jipya.

d. Tena pasteur anayepokea salaire ni chini ya amri ya wakubwa wengine. Wakubwa wale wanaweza kumsukuma kufanya maneno yasiyofaa au kugeuza mafundisho yake namna wao wanavyotaka naye anawatii kwa sababu anaogopa kama akidumu kufanya kama anafikiri Mungu anavyomwongoza kufanya, mbali na kutaka kwao, watamwondosha kwa kazi yake. Mara nyingi watu wanapima kazi ya pasteur kwa njia ya hesabu ya watu walioongezeka katika kanisa lake katika mwaka mmoja. Lakini hiki si kipimo cha kweli. Vilevile ni majaribu kwa pasteur yule kupokea katika kanisa wale wasio tayari kwanza na wasiositahili kwanza, ili kuongeza tu hesabu ya watu katika kanisa lake, watu wafikiri yeye ni pasteur mzuri. Lakini haifai kufunga mtumishi wa Bwana hivi. Inapasa awe huru kufanya kama Mungu anavyomwongoza na kumwagiza (Wagalatia 1:10).

e. Wakati kuna pasteur mmoja tu katika kanisa fulani, ni kama watu wanakusanyika kuzunguka MTU, na hawakusanyiki kwa jina la KRISTO. Kama ni pasteur anayekokota watu kwa kanisa lake, kwa sababu yeye ni mhubiri mzuri na mwongozi mzuri, halafu siku pasteur huyu atakapoondoka pale, watu wake wataondoka vilevile. Lakini kama wakikusanyika pale kwa sababu Bwana ni pale, watadumu kufika kwa sababu Yake hata kama pasteur asipokuwa.

f. Kristo ni Kichwa cha kanisa, lakini kama pasteur ni mmoja tu, watu wanamfikiri yeye kama kiongozi na kichwa na wanasahabu Kristo (Waefeso 1:22).

g. Katika Wafilipi 1:1 tunasoma ya kwamba waangalizi walikuwa kupita mmoja katika kanisa lile, si mmoja tu kwa kanisa lile au kwa kanisa lo lote lingine.

h. Hatuwezi kubisha ya kwamba wapasteur wingi ni watu wa uwezo kabisa katika kazi ya Mungu. Lakini hawakupata uwezo huu kwa sababu watu waliwachagua kuwa

wapasteur, lakini kwa sababu Mungu aliwapa zawadi hii. Ni kazi yao kutumikia watakatifu hata wao watayarishwe kwa kazi ya Mungu wao wenyewe. Waangalie sana hata Wakristo wasiwategemee wao tu, lakini wategemee Kristo.

i. Kama mtu mmoja tu akiwa na ruhusa kufundisha, kuna hatari ya kwamba Wakristo watapata mafundisho zaidi juu ya neno fulani moja au viwili tu na vitu vingine vinaachwa. Au mara nyingine anaweza kufundisha maneno yasiyo sawa na hakuna njia ya kumzuiza. Pahali Wakristo wote walipo na ruhusa ya kufundisha na wanatafuta kujua Maandiko Matakatifu na kuongozwa na Roho Mtakatifu, maneno namna hii hayatokei zaidi.

j. Tena matata mingi inakwisha kutokea vilevile kwa sababu ya watu waliochaguliwa kuwa viongozi vya makanisa nao hawakuwa wachaguliwa wa Mungu.

Hivi hata kama wapasteur wengine ni watu wa Mungu kweli na Mungu anafanya kazi Yake nao, kabisa kabisa huu si utaratibu wa Mungu kwa kanisa na si njia iliyo nzuri zaidi.

Utaratibu wa Mungu ni kwa watu wale waliopewa zawadi na Mungu kwenda kutayarisha watakatifu kwa kazi ya utumishi, na halafu nyuma kwa watakatifu wale kwenda na kufanya kazi ya utumishi. Wakati watakatifu wanapotimiza kazi yao hivi, wasioamini wataokolewa, watakatifu watajengwa, na makanisa mapya yatasimamishwa.

# WAAMINI WOTE NI MAKUHANI

Neno la saba tulilotaja kwa mwanzo wa kitabu hiki ni ya kwamba waamini wote ni makuhani kwa Mungu. Inapasa kila kanisa kushuhudia neno hili kwa njia ya kukataa namna zote nyingine za ukuhani kwa njia ya kufundisha waamini kutimiza kazi yao ya ukuhani.

1. Katika Agano la Kale kwa sheria ya Musa kabila moja tu, ndilo kabila la Lawi, na katika kabila hili jamaa ya Haruni walichaguliwa kuwa makuhani kwa taifa zima. Watu hawa walikuwa na mavazi yao mbali na watu wengine, waliweza kufanya maneno mengine watu wengine wasiyoweza kufanya, na walisimama katikati ya Mungu na watu. Wao tu waliweza kuingia katika pahali patakatifu nao tu waliweza kutoa sadaka zilizoagizwa na sheria.

2. Wakati Kristo alipofika duniani, maneno haya yote yaligeuzwa. Sasa, waamini wote ni makuhani, kama mashairi haya yanavyoonyesha:

   a. 1 Petro 2:5, "Ninyi vilevile, kama mawe yaliyo hai, mumejengwa muwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, kutoa zabihu za roho, za kupendeza Mungu kwa njia ya Yesu Kristo."

   b. 1 Petro 2:9, "Lakini ninyi ni taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe, mupate kutangaza uzuri wake ambaye aliwaita ninyi toka giza mwingie katika nuru yake ya ajabu."

   c. Ufunuo 1:5,6, "Kwake yeye ambaye alitupenda na kutuosha zambi zetu kwa damu yake, na kutufanya kuwa ufalme wa makuhani kwa Mungu na Baba yake; kwa yeye utukufu na uwezo hata milele na milele. Amina."

3. Sehemu kubwa ya kazi ya kuhani ilikuwa kutoa sadaka.

Katika Agano la Kale sadaka zilikuwa zaidi nyama waliochinjwa. Leo sadaka za mwamini ni namna nyingine:

a. Sadaka ya mwili wake (Waroma 12:1). Hii si sadaka inayokwisha kufa, lakini ni "zabihu iliyo hai, takatifu, ya kupendeza Mungu."

b. Sadaka ya mali yetu (Waebrania 13:16). "Lakini musisahau kutenda mema na kushirikiana na watu, maana sadaka kama hizi zinapendeza Mungu."

c. Sadaka ya sifa Kwake (Waebrania 13:15). "Kwa njia yake, tumpe Mungu zabihu ya sifa siku zote, ndiyo tunda la midomo inayokiri jina lake."

   Sadaka hii ya sifa iwe kwa njia mbili. Kwanza inatupasa kusifu Mungu peke yetu, na halafu inatupasa kusifu Mungu wakati tunapokutana pamoja na Wakristo wengine. Lakini ni kama sifa hii wakati Wakristo wanapokutana pamoja inakwisha kufa kwa sababu pahali pingi makusanyiko yanaongozwa na mtu mmoja tu na yanafuata utaratibu fulani. Watu wengine wanaofika wanakaa bubu tu.

4. Sadaka zetu nyingine ni maombi, ushuhuda kwa Mungu na kuchunga watu Wake. Hivi inapasa Mkristo kushinda wakati wote katika kutimiza kazi hii kubwa.

   Mafundisho yote ya Maandiko Matakatifu juu ya neno hili (Waroma 8:14; Wagalatia 5:18; Yoane 16:13) yanaonyesha ya kwamba maneno haya si kwa wakati tunapokusanyika katika nyumba ya Mungu tu, lakini ni kwa maisha yetu ya kila siku. Inatupasa sisi kuwa watu wanaofanya kazi ya ukuhani wakati wote. Kwa njia hii tutakuwa "ukuhani wa kifalme, na taifa takatifu" (Kutoka 19:6; 1 Petro 2:5-9). (Erich Sauer).

5. Hata kama waamini wote ni makuhani, kila Mkristo anahitaji kuhani yeye mwenyewe vilevile. Hitaji hili linatimizwa ndani ya Yesu Kristo. Katika Waebrania tunasoma juu Yake Aliye Kuhani letu Mkubwa anayeweza kuchukua maneno yetu ya uzaifu na aliyejaribiwa kwa njia zote kama sisi bila kutenda zambi (Waebrania 4:15).

6. Hivi inapasa kila kanisa kuheshimu Bwana Yesu kama

Kuhani mkubwa, na kufahamu ya kwamba kila mwamini ni kuhani mtakatifu na la kifalme. Lakini katika makanisa mingi hatuoni neno hili sasa. Zaidi watu wanakwisha kurudi kwa utaratibu wa Wayuda wa zamani. Hata kama wanakubali na kinywa ya kwamba Wakristo wote ni makuhani, wengi wao wanakwisha kusimamisha ukuhani wao wenyewe. Tunaona ya kuwa:

a. Watu wengine wanachaguliwa kwa kazi ya kuhubiri, kubatiza, kufunga ndoa, kuvunja mkate na kupitisha kopo, vivyo hivyo.

b. Wengine wanachaguliwa kuongoza maneno mengine katika kanisa kama kuchunga mali.

c. Watu hawa wana mavazi namna nyingine na watu wengine wa kanisa wasiochaguliwa kwa kazi fulani.

Tena mara nyingine makanisa wanafuata Wayuda wa zamani kwa njia ya kuwa na nyumba za mapambo mingi na mazabahu safi sana ndani, na vitu vingine kusaidia ndani ya kazi ya kuabudu. Wengine wanafuata utaratibu fulani unaofurahisha umtu wa watu.

Dr. C. I. Scofield anasema hivi juu ya maneno haya: "Kufananisha utaratibu wa kanisa na utaratibu wa dini ya Wayuda kunakwisha kupunguza uwezo wa Roho Mtakatifu ndani yake sana, na kulizuiza lisiendelee mbele. Kwa sababu yake kanisa linaacha pahali pake pa utengo na dunia, linasema kazi yake ni kugeuza dunia kuwa pahali pazuri zaidi, linavimbisha mali, linajenga nyumba kubwa yenye mapambo mengi, linaomba Mungu kubariki katika vita na linagawa Wakristo na wapasteur na waeskofu wanaotawala juu yao."

7. Kama kanisa fulani likifahamu maneno ya ukuhani wa Wakristo wote na kama Wakristo wakidumu katika kazi hii,

a. watu wengi watafika kwa makutano yake ya maombi na watu wataomba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu;

b. watu ndani ya kanisa lile watasaidiana na watumishi wa Bwana pahali pote duniani;

c. watu wa kanisa lile watadumu sana katika kazi ya kuhu-

biri Habari Njema, kugawa traités, kushuhudia Kristo, vivyo hivyo.

d. Mapendo yatatawala katika kanisa lile na kila mtu atakuwa tayari kusaidia wengine na mapendo na kufikiriana akihesabu wengine wazuri kuliko yeye mwenyewe.

Wakati kanisa namna hii wanapokutana pamoja, Roho Mtakatifu anatawala katika makusanyiko yao, watu wanaendelea katika zawadi za Roho ambazo Mungu aliwagawia kwa Roho Mtakatifu (1 Wakorinto 12:4-11; 14:26). Na wakati kanisa linapokusanyika hivi kuzunguka meza ya Bwana kusifu sadaka kubwa iliyotolewa kule Kalvari, sifa zao zitapanda kwa pahali patakatifu mbinguni na kupokewa na Mungu kule.

~~~~~~~~~~~~~

Tumekwisha kuangalia maneno saba makubwa tuliyotaja kwa mwanzo wa kitabu hiki. Sasa inabaki kusema juu ya maneno haya:

Ubatizo na Meza ya Bwana

Kusanyiko la maombi

Waangalizi na watumishi

Mali ya kanisa

Utumishi wa wanawake
~~~~~~~~~~~~~

# UBATIZO NA MEZA YA BWANA

Tunasoma agizo la Bwana kwa maneno haya mawili katika Matayo 28:19 na Luka 22:19,20. Tunaona watu wakiyatenda katika Matendo 10:47,48 na 20:7, na halafu tunaona maelezo juu yao katika Waroma 6:3-10 na 1 Wakorinto 11:23-32.

## Ubatizo

### A. Tuangalie kwanza maneno ya ubatizo.

Wakati tunaposemezana juu ya ubatizo, inatupasa kufahamu ya kwamba kuna namna tatu za ubatizo katika Agano Jipya.

1. **Kwanza, kulikuwa ubatizo wa Yoane** (Marko 1:4). Kama mtangulizi wa Mfalme, Yoane aliita taifa la Israeli kutubu na kuonyesha matunda yanayofaa na toba (Matayo 3:8). Wale waliofika kwake wakikiri zambi zao, walibatizwa kwa toba, na kwa njia hii walijitenga na zambi za taifa lao.

   Bwana Yesu alibatizwa na Yoane, si kwa sababu alikuwa na zambi alizohitaji kutubu lakini kwa sababu aliingia pahali pa wenye zambi waliokuwa na roho ya toba, na kutimiza haki yote (Matayo 3:15).

2. **Ubatizo wa pili ni ubatizo wa waamini** (Waroma 6:3,4). Kwa ubatizo huu Mkristo anathibitishwa na Kristo kwa kufa Kwake. Tutasemezana juu yake tena nyuma.

3. **Ubatizo wa tatu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu** (1 Wakorinto 12:13). Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa njia ya ubatizo huu waamini wote wanaunganishwa na mwili wa Kristo.

Wakati tunapofikiri juu ya batizo hizi tatu, inatupasa kukumbuka ya kwamba ubatizo wa Yoane na ubatizo wa Roho ni mbalimbali: Tunasoma juu yao katika Matayo 3:11. Vilevile ubatizo wa Yoane na ubatizo wa waamini ni mbalimbali. Kwa

Matendo 19:1-5 tunaona ya kwamba wale wanaokwisha kubatizwa na ubatizo wa Yoane walihitaji kubatizwa tena na ubatizo wa mwamini.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni mbalimbali na ubatizo wa mwamini. Watu wengine wanazania ya kwamba ubatizo wa maji ndio mfano wa ubatizo wa Roho. Lakini batizo hizi mbili ni mbalimbali kabisa. Ubatizo wa Roho unasema juu ya kuingizwa katika mwili wa Kristo, lakini ubatizo wa mwamini ni mfano wa kufa.

Hivi tukumbuke ya kwamba batizo hizi zote tatu ni mbalimbali na haifai kuzichanganya.

**B. Nyuma ya siku ya Pentekote tunasoma ya kwamba waamini tu walipata ubatizo.** Ona maneno haya:

. 1. "Nao waliopokea neno lake kwa furaha wakabatizwa" (Matendo 2:41).

2. "Lakini wakati walipoamini Filipo, akihubiri Habari Njema ya ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake" (Matendo 8:12).

Ndiyo, mara nyingine tunasoma juu ya watu wote wa nyumba moja wakipata ubatizo (Matendo 16:15 na 1 Wakorinto 1:16), lakini hatuoni ya kwamba katika nyumba hizi kulikuwa na watoto wasioamini Bwana Yesu bado.

**C. Tunaona maneno ya ubatizo wa mwamini wazi zaidi katika Waroma 6:1-10.** Tunaweza kujumlisha mafundisho ya mashairi haya hivi:

1. Wakati Kristo alipokufa, mawimbi yote ya hasira ya Mungu yalipita juu Yake (Zaburi 42:7).
2. Alikufa kwa pahali petu.
3. Kwa sababu alikufa kama Mkombozi wetu, tunaweza kusema ya kwamba wakati Yeye alipokufa, sisi tulikufa vilevile.
4. Kwa njia ya kufa Kwake alitimiza kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wa watu mara moja.

5. Hivi sisi vilevile tunakwisha kufa kwa zambi. Zambi haina amuri juu yetu tena.
6. Mungu anaona kila mwamini kama mtu aliyesulibishwa pamoja na Kristo. Desturi zake zote kama mtu wa zamani zinakwisha kufungwa kwa msalaba.
7. Kwa njia ya ubatizo mwamini anaonyesha kitu kinachokwisha kufanyikana. Kwa njia ya kuingia ndani ya maji na kufunikwa nayo anasema, "Kwa sababu ya zambi zangu nilistahili kufa. Lakini wakati Yesu alipokufa, mimi nilikufa vilevile. Mtu wangu wa zamani, tabia yangu ya zamani, ilisulibishwa pamoja naye. Wakati Yesu alipozikwa, mimi nilizikwa vilevile, na sasa ninakiri ya kwamba haifai kwa mtu wangu wa zamani kuonekana kwa Mungu tena katika maisha yangu ya kila siku."
8. Halafu kama Yesu alivyofufuka toka wafu, vivyo hivyo mwamini anatoka katika maji ya ubatizo. Kwa njia hii anaonyesha ya kwamba anakusudi kutembea katika upya wa uzima. Hataishi tena kwa yeye mwenyewe tu, lakini ataweka maisha yake mikononi mwa Mwokozi ili Yeye aweze kuishi na kujionyesha ndani yake.

Hivi tunaweza kusema ya kwamba ubatizo unaonyesha ya kwamba mwamini anaachana na maneno yake ya zamani. Kwa njia yake anatii Bwana waziwazi mbele ya watu wote (Matayo 28:19,20) na analeta mfano wa mauti ya mwamini pamoja na Kristo. Ubatizo hauwezi kuokoa. Ni kwa wale tu wanaokwisha kuokolewa.

D. **Kuna mabishano mingi juu ya namna gani inapasa kubatiza,** au kwa njia ya kumwanga maji nusu tu juu ya kichwa cha mtu au kwa njia ya kuingiza mwili wake mzima katika maji. Labda maneno tutakayosema sasa yatatusaidia kufahamu vizuri.

1. Neno hili "batiza" linatoka kwa neno la Kiyunani, maana yake "kuingiza katika maji, kunawa."
2. Wakati tunaposoma juu ya ubatizo wa Kristo, tunasoma, "Wakati Yesu alipobatizwa, mara moja alitoka katika maji" (Matayo 3:16).

3. Yoane yeye mwenyewe alikuwa akibatiza kwa Ainoni kwa sababu maji **mingi** yalikuwa pale (Yoane 3:23).

4. Wakati towashi la Etiopia alipobatizwa, Maandiko Matakatifu yanaonyesha ya kwamba **"wakatelemuka wote wawili ndani ya maji,** Filipo na yule towashi; akambatiza. Kisha **walipotoka katika maji,** Roho ya Bwana akanyakua Filipo..." (Matendo 8:38,39).

5. Tunakwisha kuona mbele (Waroma 6:3) ya kwamba ubatizo ni mfano wa kuzika. Kumwanga nusu ya maji juu ya kichwa cha mtu hakutuleti kufikiri juu ya kuzika, lakini kuingiza mwili mzima katika maji kunaonyesha neno lenyewe wazi sana.

E. **Lakini haifai kubatiza tu mtu namna Kitabu cha Mungu kinavyoonyesha.** Kitu kikubwa zaidi ni kama mtu akiwa na roho gani wakati anapobatizwa. Kuna elfu za watu wanaokwisha kubatizwa, miili yao mizima kuingizwa katika maji, lakini kabisa kabisa hawayabatizwa bado. Mtu aliyebatizwa kweli kweli ni mtu anayeonyesha katika maisha yake ya kwamba mtu wake wa zamani anakwisha kuwekwa kwa pahali pa mauti. Ubatizo si ushuhuda wa inje tu, ni wa roho vilevile.

F. **Watu wengine wanafikiri ya kwamba pasteur tu** anaweza kubatiza mtu. Sivyo. Kila mtu aliye mwamini anaweza kubatiza watu wengine.

G. **Kwa wakati wa mwanzo wa kanisa** wakati mwamini alipobatizwa, mara nyingi alipata mateso na mara nyingine aliuawa nyuma ya siku chache. Lakini wakati watu wengine walipookolewa, mara moja walikuwa tayari kuingia kwa pahali pa wale waliouawa, wakabatizwa vilevile.

Hata wakati wa sasa, katika pahali pengine ubatizo ni mwanzo wa mateso makali sana kwa mwamini. Kwa inchi nyingine wakati mtu anapokiri tu jina la Kristo na kinywa watu wanamwacha na salama, lakini wakati anapokiri Kristo wazi kwa njia ya ubatizo na hivi kuachana na maneno yake ya zamani, adui za msalaba wa Kristo wanaanza kupiga vita naye.

Lakini hata kama kuna mateso, kila mtu anayebatizwa atapata furaha namna towashi la Etiopia alivyopata na atakwenda zake na furaha.

## Meza ya Bwana

A. **Meza ya Bwana ilisimamishwa na Bwana Yesu usiku alipotolewa mikononi mwa adui Zake.** Mara moja nyuma ya kula Pasaka pamoja na wanafunzi Wake alisimamisha neno hili tunalojua kama Meza ya Bwana sasa. "Akatwala mkate, akashukuru, akavunja, akawapa, akisema: Huu ni mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi. Na tena kikombe nyuma ya kula, akisema: Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu inayomwangika kwa ajili yenu (Luka 22:19,20).

B. Wakati tunapofikiri juu ya maana ya meza ya Bwana, inatupasa kukumbuka maneno mane:

1. **Ni wakati wa ukumbusho.** Mwokozi alisema, "Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi." Ni wakati wa kukumbuka mateso Yake na mauti Yake, namna alivyotoa mwili Wake na kumwanga damu Yake. Hapa tunakumbuka maneno yote ya Kalvari.
2. **Haiwezekani kwa sisi kukumbuka mateso ya Bwana Yesu pasipo mioyo yetu kujaa na kuabudu na sifa.** Hivi meza ya Bwana ni wakati wa kuabudu Mungu kwa uzuri Wake na ukubwa Wake na kwa maneno yote ambayo alitufanyia.
3. **Tena meza ya Bwana ni ushuhuda mbele ya watu wa umoja wa mwili wa Kristo, waamini wote wa kweli.** Kwa njia ya kutwaa mkate mwamini anashuhudu umoja wake pamoja na kila mtoto wa kweli wa Mungu. Kwa njia ya kunywa kikombe, anakiri umoja wake pamoja na kila mtu anayekwisha kusafishwa na damu ya damani ya Kristo (1 Wakorinto 10:16,17).
4. **Na tena meza ya Bwana inatukumbusha kila mara ya kwamba Yeye ambaye aliisimamisha, ndiye Bwana Yesu, atarudi tena.** Kwa sababu kila mara munapokula

mkate huu, na kunywa kikombe hiki, munatangaza kufa kwa Bwana hata atakapokuja (1 Wakorinto 11:26).

Hivi mwenye kuabudu anatazama nyuma kwa Golgota na kukumbuka Kristo katika mauti Yake, na vilevile anaangalia juu kwa kiti cha ufalme cha Mungu na anamsifu kwa kazi ya ukombozi, na tena anatazama mbele kwa wakati Bwana atakaposhuka toka mbinguni kupeleka watu Wake Kwake.

C. **Maandiko Matakatifu hayaagizi mara ngapi au wakati gani inatupasa kukutana.**

1. Katika Matendo 20:7 tunasoma ya kwamba "Siku ya kwanza ya juma, wakati wanafunzi walipokutana kuvunja mkate..." Siku ya kwanza ya juma ni siku ya Bwana. Ni siku Bwana Yesu alipofufuka na ni siku nzuri kwa watu Wake kukutana pamoja kumwabudu na kumkumbuka.
2. Katika 1 Wakorinto 11:26 tunasoma, "Kila mara munapokula mkate huu na kunywa kikombe hiki..." Haisemi "kila juma" au "kila mwezi". Hata hivi tunafikiri wakati wa mwanzo wa Kanisa Wakristo walikutana kukumbuka kufa kwa Bwana kila juma. Ni kitu kizuri kutakasa kila siku ya Bwana kwa njia ya kuzunguka meza Yake na kukumbuka kufa Kwake. Lakini katika Biblia hakuna agizo mara ngapi inatupasa kukutana kwa kuvunja mkate.

D. **Meza ya Bwana ni kwa Wakristo tu.** Wakristo tu wanaweza kufahamu maana yake. Tena Wakristo sharti wajihukumu wenyewe mbele ya kufika kwa meza ya Bwana (1 Wakorinto 11:28). Sharti wakiri zambi zao na kuziacha mbele ya kufika kwa meza, na vilevile inawapasa kula mkate na kunywa mvinyo kwa utaratibu (1 Wakorinto 11:21,22). Wote wanaokula na kunywa bila kujihukumu wenyewe ni katika hatari ya azabu ya Bwana (1 Wakorinto 11:27,29-32).

E. Tukumbuke vilevile ya kwamba **inawezekana kula mkate na kunywa mvinyo kwa desturi tu bila kufikiri juu ya maana yake.** Sharti tutembee karibu na Bwana, halafu tutaweza kumkumbuka kweli kweli.

# KUSANYIKO LA MAOMBI

**1. Hatupati habari nyingi katika Agano Jipya juu ya makusanyiko ya kanisa la pahali fulani**. Tunajua ya kwamba Wakristo walikutana kwa ushirika, maombi, mafundisho kutoka kwa Kitabu cha Mungu na kuvunja mkate (Matendo 2:42). Hatusomi juu ya makusanyiko mengine. Hatusomi ya kwamba kanisa lilikuwa na kusanyiko kwa kutangaza Habari Njema. Ni kama kazi hii ilikuwa kazi ya kila Mkristo mmoja mmoja pahali wapi alipoweza kupata wasioamini tayari kumsikia. Halafu Wakristo walileta wale walioamini kwa kanisa.

**2. Katika makusanyiko yote ya makanisa kwa wakati wa mwanzo kusanyiko la maombi lilionekana zaidi.** Ndiyo, kanisa lilizaliwa nyuma ya kusanyiko la maombi (Matendo 1:14), na nyuma yake Wakristo walidumu katika maombi (Matendo 2:42). Katika historia nzima ya Kanisa tangu mwanzo tunaona faida kubwa ya watu waliodumu katika maombi.

**3. Mungu anakubali kwa sisi kukutana pamoja kwa kuomba pamoja.** Hakubali tu, lakini analeta ahadi ya kwamba Yeye Mwenyewe atakuwa katikati yetu. Katika Matayo 18:19 na 20 tunasoma,

> "Ninawaambia ninyi tena, ya kwamba wawili katikati yenu watakapopatana duniani kwa kitu cho chote ambacho wataomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa pahali watu wawili au watatu wanapokusanyika kwa jina langu, mimi ni pale katikati yao."

Mashairi haya ni wazi kabisa. Kwanza kama Wakristo wawili wakifungana pamoja juu ya ombi fulani, Mungu atajibu ombi lile. Tena wakati Wakristo wanapokutana kwa jina la Bwana Yesu, Yeye ni pale katikati yao.

Lakini ni kama sisi hatuamini maneno haya. Kama tungaliamini kama makusanyiko yetu ya maombi yangalijaa na watu na kama makanisa yetu yangaliwaka kwa Mungu.

**4.** Wakati tunapofikiri juu ya kusanyiko la maombi la Wakristo, tukumbuke maneno machache kwanza.

**A**. Katika kusanyiko la maombi mtu mmoja anaomba na sauti. Wengine wananyamaza, lakini kabisa kabisa wote wanaomba. Sauti ya mtu mmoja inasikiwa naye anataja wazi maombi ya watu wale wote. Wengine wanafuata maombi yake na masikio yao na mara nyingi wanaonyesha ya kwamba wanashiriki pamoja naye ndani yao kwa njia ya kusema "Amina".

**B**. Kitu kikubwa ambacho inatupasa kukumbuka ni kuomba na roho ya kweli. Maombi mengi ni maombi ya kinywa tu lakini roho ya mtu yule anayeomba si ndani ya maombi yake. Kabisa kabisa hataki maombi yale anayoomba yatimie. Kwa mfano mara nyingine mtu anaomba Mungu mbele ya watu wengine kumsafisha na kumwonyesha zambi zake na kumkokota karibu naye, lakini kama angalijua ya kwamba itapasa Mungu kumletea taabu kusudi ombi hili litimizwe kama asingaliomba hivi. Maombi namna hii, ya kinywa tu, bila roho ya kweli, hayawezi kufika kwa Mungu. Mara nyingi Wakristo wanapata desturi kwa maombi yao, masemo fulani, maombi fulani, lakini maombi yale hayana faida kwa Mungu wala kwa watu.

**C**. Hatari nyingine ni maombi marefu. Ndiyo, Kitabu cha Mungu kinatuagiza kuomba pasipo kuacha, lakini maana ya shairi hili si kusema mtu mmoja amalize saa nzima ya kusanyiko la maombi. Ni vizuri zaidi kila mtu aombe kwa ufupi, hivi watu wengi wataweza kuomba.

**D**. Tena tusitaje maneno "en général". Tutaje kitu wazi. Kwa mfano, tusiombe, "Mungu, okoa watu wa dunia nzima," lakini tuombe, "Mungu, okoa ndugu yangu Daudi." Halafu wakati Daudi anapookolewa, utajua Mungu anakwisha kujibu maombi yako na utapata hamu kuombea watu wengine vilevile.

**5**. Haifai kwa kusanyiko la maombi kuwa kitu cha kukauka pahali watu wanaposhindwa na usingizi! Kuna maneno mengi tunayoweza kuweka mbele ya Mungu kwa maombi. Tunataja mengine hapa:

**A.** Omba kwa wale ambao wanatutawala inchini mwetu tukiwataja na majina yao. Tuombe waweze kuokolewa, na hata tuweze kuishi na salama chini ya utawala wao (1 Timoteo 2:2).

**B.** Tuombee wale walio wagonjwa katika kanisa letu. Bwana anajua wanani ndio wagonjwa, lakini labda kuna Wakristo wengine wasiojua, hivi tutaje majina yao katika maombi yetu.

**C**. Tuombee ndugu zetu na rafiki zetu wasiookolewa bado. Haifai sisi kuwa na haya wakati tunaposikia majina ya wapenzi wetu katika kusanyiko la maombi. Kama tukitaka kweli kweli waokolewe, tutafurahi kwa kanisa kushiriki pamoja nasi kwa maombi kwa ajili yao.

**D**. Tuombee wazee wa kanisa. Wana kazi kubwa na wanahitaji akili na saburi. Wanahitaji maombi yetu.

**E**. Tuombee wahubiri wanaokwisha kutoka katika kanisa letu. Tujaribu kupata habari zao ili tuweze kujua mahitaji yao na kuwaombea na akili.

**F**. Tuombee Ecole du Dimanche, kwa kiongozi, kwa walimu, na kwa watoto wanaofundishwa Neno la Mungu.

**G**. Tuombee wamasikini. Kwa sababu labda wengine wanaweza kuwa na haya, tusitaje majina yao.

**H**. Tuombee wanaume na wanawake wa kanisa letu waliohama pahali pangine.

**I**. Tuangalie tuwe na mashukuru katika maombi yetu vilevile. Tunaona neno hili wazi katika Wafilipi 4:6. Bwana anataka watu Wake kumshukuru. Kukaa bila asante kwa rehema Zake zote kwetu ni zambi.

**6**. Kuna maneno mengine yanayohitajiwa ili maombi yetu yapate jibu? Kabisa!

**A**. **Sharti tukae ndani ya Kristo.** Yesu alisema, “Kama mukikaa

ndani yangu, na maneno yangu yanakaa ndani yenu, mutaomba neno gani munalotaka, na mutafanyiziwa" (Yoane 15:7). Kukaa katika Kristo ni kutii maagizo Yake, kufanya mapenzi Yake na kufuata Neno Lake.

**B.** Neno la pili, **sharti maombi yetu yapatane na mapenzi Yake.** "Na huu ndio uhodari tulio nao mbele yake, ya kama tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, anatusikia" (1 Yoane 5:14). Katika Kitabu cha Mungu tunaona maombi gani yanapatana na mapenzi Yake. Kwa mfano haifai kijana Mkristo kuomba Mungu kubariki ndoa yake na msichana msiyeamini, kwani Kitabu cha Mungu kinaonyesha waziwazi ya kwamba Mungu hataki Mkristo na msiyeamini kufungana pamoja katika ndoa.

**C. Sharti maombi yetu yawe kwa jina la Kristo.**

"Kila neno munaloomba Baba kwa jina langu atawapa ninyi" (Yoane 16:23).

"Na mukiomba lo lote kwa jina langu, nitalifanya, Baba atukuzwe ndani ya Mwana" (Yoane 14:13).

Kama tukiomba kweli kwa jina Lake, ni sawasawa Yeye Mwenyewe anaomba kitu hiki karibu na Baba Yake.

**D**. Halafu neno la mwisho, **makusudi ya maombi yetu yawe safi.** Yakobo anatukumbusha ya kuwa mara nyingine tunaomba na hatupokei kitu tunachoomba kwa sababu hatuombi vizuri lakini tunaomba kwa faida yetu wenyewe (Yakobo 4:3). Kama maombi yetu ni kwa faida yetu wenyewe, na si kwa utukufu wa Mungu, Mungu hatayajibu. Kwa mfano: Kama nikiomba Mungu kunipa mali nyingi, kusudi niweze kununua vitu vingi ninavyotaka, Mungu hatajibu maombi yangu, lakini kama nikiomba Mungu kunipa mali niweze kutumika nayo kazi Yake, atanipa kama kazi hii ninayotaka kufanya inapatana na mapenzi Yake.

**7.** Tena mbele ya kumaliza sura hii kuna maneno machache mengine tunayotaka kusema juu yao ili makusanyiko yetu ya maombi yawe makusanyiko ya uwezo kabisa.

**A. Usiombe kwa kuonekana mbele ya watu**. Kumbuka wada-

nganyifu wanapenda kusimama na kuomba maombi marefu kwa kuonekana mbele ya watu (Matayo 6:5).

B. **Usiombe Mungu kufanya kitu unachoweza kufanya wewe mwenyewe.** Kwa mfano tunaomba Mungu kuleta wasioamini kwa makusanyiko yetu ya Habari Njema. Hatajibu maombi haya, kwani ni kazi yetu kwenda kuwaita na kuwaleta sisi wenyewe. Lakini tunaweza kuomba Mungu kuwakubalisha wakati tunapokwenda kuwaita.

C. Angalia vilevile **usiombe kitu unachojua si vizuri kwa wewe kupata.** Mara nyingine Mungu anakubali maombi namna hii, lakini pamoja na kukubali anatuma baridi kwa roho (Zaburi 106:15).

D. **Usichoke kama Mungu hajibu mara moja.** Kuna baraka ndani ya kumngojea na jibu Lake haliwezi kufika nyuma kupita kipimo na kuharibu imani yako.

E. Tena, kama mara nyingine Mungu hajibu namna ulivyoomba, **kumbuka ya kwamba Bwana ana ruhusa kutupatia sisi kitu kizuri kuliko kitu kile tulichoomba Kwake.** Sisi hatujui nini ni vizuri kwa sisi, lakini Yeye anajua, naye anatuletea sisi kupita tulivyoweza kufikiri au kuomba.

Mbele ya kumaliza sura hii tuseme waziwazi ya kwamba kanisa lisiloomba haliwezi kuendelea. Hata kama tunaweza kukutana kwa desturi, matunda ya kweli hayatakuwa bila maombi. Kanisa lisiloomba ni kanisa linalokwisha kupoa kabisa.

# WAZEE

Hapa tunataka kusemezana juu ya watu wanaochaguliwa kuangalia kundi la Mungu. Si wazee kila mara kwa njia ya miaka.

**1. Waangalizi, wazee na wasimamishi ni watu wanaofanya kazi moja, ndiyo kuchunga kundi la Mungu** (1 Timoteo 3:1; Matendo 20:28 na Matendo 20:17). Tuangalie kwanza namna gani wazee wanachaguliwa.

**A.** Ni Roho Mtakatifu tu anayeweza kufanyiza mtu kuwa mzee (Matendo 20:28). Hata kama kanisa linaweza kukutana kwa kuchagua wazee, wao hawawezi kuweka roho ya mzee ndani ya mtu.

**B.** Utaratibu wa Mungu ni kwa Mungu kufanyiza watu kuwa wazee, kuwatayarisha kwa kazi hii, na halafu wao wanafanya kazi yenyewe hata wakati wasipoitwa bado wazee, kisha Wakristo wa kanisa wanaona na kufahamu ya kwamba huyu ndiye mzee anayekwisha kuchaguliwa na Mungu na halafu wao vilevile wanamheshimu kama mzee.

**C.** Ni kweli ya kwamba Paulo na wengine walichagua wazee (Matendo 14:23; Tito 1:5), lakini kwa wakati ule watu hawakuwa na Agano Jipya zima bado, na hawakuweza kujua kama inapasa mzee kuwa mtu wa namna gani, na halafu walihitaji kutegemea akili ya mitume au ya wale waliotumwa na mitume.

Tuone vilevile ya kwamba Paulo hakuchagua wazee mara ya kwanza alipofika kwa kanisa fulani. Aliacha saa kwa wazee wale waliochaguliwa na Mungu kuonekana kwa njia ya kazi yao, na halafu aliwaonyesha wazi kwa kanisa na kuwaita wazee.

**2. Biblia inatupasha wazi nini inahitajiwa ndani ya mzee.** Ona 1 Timoteo 3:1-7 na Tito 1:5-9.

**A.** Sharti awe mtu asiye na laumu. Haiko kusema atakuwa mtu pasipo zambi, lakini mtu asiyeweza kusitakiwa na kitu mbele ya watu. Maneno yake yote ni taratibu.

**B.** Sharti awe mume wa mke mmoja. Wengine wanafikiri maana ya neno hili ni kusema sharti awe mtu anayekwisha kuoa. Wengine wanafikiri ni kusema haifai awe na wake kuliko mmoja. Neno lile ni wazi, ndilo ya kwamba haifai kwa mzee kwamba na mke kuliko mmoja, lakini hatuwezi kusema na nguvu yote ya kwamba sharti mzee awe na mke. Hatujui.

**C.** Sharti awe mwenye kiasi. Afanye kila kitu kwa kipimo kizuri, si kupita kipimo.

**D**. Sharti awe mtu mwema anayefanya maneno yote na utaratibu. Desturi ovyo ovyo hazifai kwa mzee.

**E**. Sharti awe mtu anayefurahi kukaribisha wageni. Mlango wa nyumba yake utakuwa wazi kwa watumishi wa Bwana. Na nyumba yake itakuwa kama nyumba ya Lazaro, Maria na Marata kwa Betania pahali Bwana Yesu alipopenda kukaa.

**F.** Sharti mzee ajue kufundisha. Hata kama labda hatakuwa na zawadi ya kufundisha Neno la Mungu zaidi zaidi, inampasa kujua Neno la Mungu aweze kusaidia waamini nalo wakati wanapohitaji kusaidiwa.

**G.** Haifai awe mtu wa kulewa na mvinyo au mtu wa kupiga watu. Mtu anayepiga mtumishi hastahili kwa kazi ya mzee.

**H.** Asiwe mtu wa kutamani mali. Mzee wa kweli atafahamu ya kwamba mali ni kwa kazi ya Bwana tu na kwa kuendelesha kazi Yake. Haifai Mkristo kutamani mali kwa yeye mwenyewe. Kutamani ni kama kuabudu sanamu.

**I.** Sharti awe mtu wa saburi. Bwana yake alikuwa mpole, na mtumishi hapiti bwana yake. Labda watu wa dunia hawawezi kuheshimu watu wapole na wenye saburi, lakini kwa macho ya Mungu wao ni watu wa faida.

**J.** Asiwe mtu wa magomvi.

**K**. Sharti mzee atawale nyumba yake vizuri na watoto wake wamtii. "Kwa maana mtu asiyejua kusimamia nyumba yake

mwenyewe, atachunga kanisa la Mungu namna gani?” (1 Timoteo 3:5).

**L.** Haifai awe Mkristo wa sasa tu. Wala hatufikiri tu hesabu ya miaka anayokwisha kuishi hapa duniani. Sharti mzee awe mtu anayekwisha kuishi siku nyingi kwa imani, anayekwisha kuendelea na kujua Mungu, anayekwisha kuwa mwanamume **kwa imani**. Mkristo wa sasa akipewa kazi ya mzee, mara nyingine atapata majivuno zaidi na ataanguka.

**M**. Sharti awe na ushuhuda mzuri mbele ya wasioamini. Sharti wao wajue huyu ni mtu wa haki, mtu mwema.

**N.** Haifai awe mtu wa kutaka kutimiza mapenzi yake mwenyewe tu. Haifai awe mtu wa kukasirika mbio. Sharti awe mtu anayependa yaliyo mema. Sharti awe mtakatifu na mwenye haki. Sharti ashike neno la imani, ndilo Neno la Mungu na kusimamia imani.

Au kwa ufupi tunaweza kusema sharti mzee awe mtu anayejua kujitawala mwenyewe, na anayejua kutawala nyumba yake, na anayesimamia kweli ya Mungu.

Kitabu cha Mungu hakisemi ya kwamba mzee sharti awe mtu anayekwisha kujifunza sana, au anayekwisha kuwekewa mikono kuwa pasteur. Hakisemi ya kwamba sharti awe mwenye mali nyingi, au mtu wa kuonekana vizuri, au mtu wa kujulikana katikati ya watu. Hata kama yeye ni kiwete na masikini, hata kama anafanya kazi ya chini tu kwa kusaidia mahitaji ya nyumba yake, anaweza kustahili kazi ya mzee kama roho yake mbele ya Mungu ni safi na anatimiza maneno haya tunayokwisha kutaja. Mara nyingi tunaanguka kwa sababu tunampa mtu kazi ya mzee kwani ni mtu wa heshima katikati ya watu, mtajiri, vivyo hivyo, lakini kwa roho yeye ni masikini na uwezo wa Roho Mtakatifu si ndani yake.

**3. Kazi ya mzee ni nini ?**

**A.** Kazi yake ya kwanza ni kukulisha kundi la Mungu (1 Petro 5:2: Matendo 20:28). Anafanya hivi kwa njia ya kufundisha Neno la Mungu. Anaweza kufanya hivi kwa njia ya kufundisha kanisa zima, au kwa njia ya kwenda kuangalia

watu katika nyumba zao na kuwafundisha sawasawa na mahitaji yao. Hili ndilo neno kubwa sana.

**B**. Neno la pili, inampasa kufanya kazi ya msimamishi. Petro anaandika katika 1 Petro 5:2, "Mukiwasimamia". Maana yake nini?

1. Maana yake haiko kusema atafanya kazi hii kwa sababu analazimishwa kuifanya, lakini kwa sababu anataka.
2. Maana yake haiko kusema ataifanya kwa kupata mali, "si kwa feza ya uchafu, lakini kwa nia tayari."
3. Maana yake haiko kutawala watu wa Mungu. Mzee si mtawala.
4. Lakini maana yake ni yeye atakuwa mfano kwa kundi ndilo Wakristo. Inapasa mzee kukumbuka ya kwamba Mchungaji Mwema, ndiye Yesu Kristo, hasukumi kondoo Zake, lakini anawaongoza. Anakwenda mbele yao. Inapasa kila mzee aliye mchungaji wa kundi vilevile chini ya Bwana Yesu kufanya vivyo hivyo. Si kazi yake kutoa maagizo, na sharti watu wamtii. Sivyo. Atasimamia kanisa kwa njia ya mwenendo wake safi na mfano wake mzuri.

**C.** Wazee wana kazi kubwa sana kwa kanisa. Kama wazee wakiwa watu wa Mungu kabisa wanaoweka Bwana kwanza katika maisha yao, wanaoonyesha neema ya Bwana Yesu, kanisa vilevile litakuwa kanisa hai linaloendelea vizuri kwa maneno ya Bwana na kuwaka kwa Roho Mtakatifu. Lakini kama wazee wakiweka mafikiri yao zaidi juu ya maneno ya dunia, na hawana saa kusoma Kitabu cha Mungu na kuomba utaona Wakristo wa kanisa lile watakuwa baridi vilevile.

**D**. Tena ni kazi ya mzee kusaidia wale walio zaifu. "Nimekwisha kuwaonyesha ninyi mfano katika maneno yote, ya kwamba imetupasa kutenda hivi na kusaidia wazaifu, na kukumbuka maneno ya Bwana Yesu, kama alivyosema: Heri ya kutoa inapita heri ya kupokea" (Matendo 20:35).

Mara nyingi tunafikiri inapasa wazee **kupata** kitu kwa sababu ya kazi yao, lakini sivyo. Ni kazi yao kusaidia wale walio na mahitaji kwa njia ya kuwapa ya mali yao.

**E.** Kazi ya mzee ni kuhamakia, kukemea na kuonya (2 Timoteo 4:2; Tito 1:13; 2:15). Kitu cho chote kisichopatana na Neno la Mungu sharti kihamakiwe na nguvu. Halafu wale wasiotaka kusikia sharti wakemewe na kuonywa. Sharti mzee asimame na nguvu kwa kweli ya Mungu.

**4**. Halafu kanisa litatendea wazee namna gani? Kwa 1 Timoteo 5:17,18 tunaona waziwazi ya kwamba wazee wengine wanasaidiwa na kanisa kwa njia ya mali kwa mahitaji yao.

"Wazee wanaotawala vema wahesabiwe kustahili heshima mara mbili, zaidi wale wenye kujitaabisha sana kwa neno na kwa mafundisho. Kwa sababu maandiko yanasema: 'Usifunge kinywa cha ngombe wakati anapokanyaga ngano;' na tena: Mtenda kazi anastahili mshahara wake."

Tunaona waziwazi vilevile ya kwamba wengine walitumika kazi ya biashara kwa mahitaji yao wenyewe. Paulo yeye mwenyewe alifanya hivi (1 Wakorinto 4:12).

Haifai kuhamakia mzee, lakini kumwonya kama **baba** (1 Timoteo 5:1). Mashitaki yakiwa juu ya mzee, sharti washuhuda wawe wawili au watatu (1 Timoteo 5:19).

Inapasa watu wa kanisa kuheshimu na kutii **wazee**.

"Muwaheshimu sana katika mapendo kwa ajili ya kazi yao" (1 Watesalonika 5:13).

"Kumbukeni waongozi wenu ambao waliwaambia ninyi Neno la Mungu; na kuangalia mwisho wa miendo yao, fuateni imani yao. Yesu Kristo ni sawasawa, jana, leo na hata milele" (Waebrania 13:7,8).

**5**. Kwa mwisho tunaona zawabu ya wazee.

"Na wakati Mchungaji mkubwa atakapoonekana, mutapokea taji ya utukufu isiyoharibika" (1 Petro 5:4).

# WATUMISHI

Wakati tuliposoma juu ya wazee tuliona ya kwamba kazi yao ni kuchunga kundi la Mungu kwa njia ya Neno Lake na kuwaongoza kwa njia Yake. Tuliona vilevile ya kwamba katika kanisa moja kuna wazee kuliko mmoja.

Sasa tuangalie kazi ya "Watumishi".

**1.** Tuone watumishi wengine katika Kitabu cha Mungu. Mtu anayesaidia ndani ya kazi ya utawala na kuchunga utaratibu wa inchi anaitwa mtumishi wa Mungu (Waroma 13:4). Foibe aliitwa mtumishi wa kanisa lililo katika Kenkurea (Waroma 16:1). Kristo Yeye Mwenyewe aliitwa mtumishi wa tohara katika Waroma 15:8. Tunafikiri juu ya watu wale katika Matendo 6:1-6 waliopewa kazi ya kugawa mali na jina hili vilevile, lakini kazi ya mtumishi si kazi ya kugawa mali tu.

**2.** Hata kama Kitabu cha Mungu hakitaji waziwazi kazi ya watumishi, kinatuonyesha waziwazi nini inahitajiwa ndani ya mtumishi. Kwa 1 Timoteo 3 kuanza na shairi 8 tunasoma,

> "Hivi watumishi wanapaswa kuwa watu wa utaratibu, si wenye kusema maneno kwa hila, si watu wa kutumia mvinyo nyingi, si wenye choyo ya feza chafu; wakishika siri ya imani katika zamiri safi. Na hawa wajaribiwe kwanza; kisha watumike kazi ya watumishi kama wakikwisha kuonekana pasipo laumu. Hivi wanawake wawe watu wa utaratibu, si wasingiziaji, wenye kiasi, waaminifu katika maneno yote. Watumishi wawe kila mtu mume wa mke mmoja, wakisimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa sababu wenye kutenda kazi ya watumishi vizuri wanajipatia alama nzuri na uhodari sana katika imani iliyo katika Kristo Yesu."

**A.** Hapa tunaona ya kwamba k**itu cha kwanza kinachohitajiwa ni utaratibu.** Watu hawataamini mtu anayetenda maneno ovyo ovyo.

B. **Sharti mtumishi awe mtu wa kusema haki, si kwa hila.** Asiseme kitu kimoja kwa mtu mmoja na kitu kingine kwa mtu mwingine. Zaidi kama ni kazi yake kuchunga mali, namna anazichunga iwe haki na wazi kwa watu wengine, wasiwe na shaka.

C. **Haifai awe mtu wa kutumia mvinyo nyingi**. Hakuna mtu anayeamini mlevi. Tunakwisha kuona tena na tena ya kwamba kulewa kunaharibu uwezo wa mtu kufanya kitu taratibu na kunaharibu ushuhuda wake kwa Mungu naye hana faida tena kwa kazi Yake.

D. **Haifai atamani mali.** (Mingi ya maneno haya ni maneno yanayohitajiwa kwa mzee vilevile.) Tamaa ya mali ni mtego. Kama mtu akiweka roho juu ya kujipatia mali hawezi kuweka roho yake yote juu ya kazi ya Bwana. Hivi kazi yake kwa Bwana itakuwa ovyo ovyo na Mungu hataipokea.

E. **Sharti mtumishi ajue kweli ya Mungu na kuitenda vilevile**. Sharti awe na zamiri safi mbele ya Mungu. Himeneo na Alesanduro walijua kweli ya Mungu vilevile, lakini walikologana na zambi – ndiyo mafundisho yasiyo sawa (2 Timoteo 2:17). Walinyamazisha zamiri zao, na wameharibisha imani (1 Timoteo 1:19,20). Ni kitu kizuri sana kuwa na damiri teketeke.

F. Halafu tunasoma, "**Na hawa wajaribiwe kwanza;** kisha watumike kazi ya watumishi kama wakikwisha kuonekana pasipo laumu" (sh. 10). Pahali pengine tunasoma, "Usiwekee mtu mikono kwa haraka" (1 Timoteo 5:22). Sisi sote tunahitaji maonyo haya. Wakati tunapokutana na mtu mara ya kwanza tunafikiri yeye ni mtu mzuri sana, na mbio mbio tunampa kazi. Halafu nyuma tunafahamu ya kwamba tulitenda kwa haraka. Yeye si mzuri kwa njia zake zote kama tulivyofikiri.

G. **Tena sharti mke wa mtumishi atimize maneno mengine** vilevile kama bwana yake atafanya kazi ya mtumishi. Kwa nini? Tunajua ya kwamba mke anaweza kusaidia bwana yake sana katika kazi yake kwa Mungu, au anaweza kumzuiza. Kwa njia ya kuleta magomvi na mabishano anaweza kuharibu kazi yake kabisa. Kwa hivi Maandiko Matakatifu yanasema, "Hivi wanawake wawe watu wa utaratibu, si wasingiziaji, wenye kiasi, waaminifu katika maneno yote" (1 Timoteo 3:11).

**H.** Kama tulivyoona juu ya mzee, **inapasa mtumishi kuwa na mke mmoja tu na kutawala watoto wake na nyumba yake vizuri.** Kama tulivyosema mbele, kama mtu asipoweza kutiisha watu wa nyumba yake, namna gani ataongoza Kanisa la Mungu?

**3. Mtumishi anapata zawabu kwa njia mbili.** Kama mtumishi akifanya kazi yake vizuri anajipatia salama nzuri. Maana yake ni kusema atakuwa na heshima katikati ya Wakristo na atapata zawabu wakati Kristo atakapojaribu kazi ya kila mtu.

Neno la pili, atakuwa na uhodari sana katika imani. Ndiyo, kwa macho ya watu wa dunia neno hili ni kitu bule. Hawawezi kulifahamu. Lakini kwa mtoto wa Mungu ni kitu cha damani sana.

Halafu kwa njia ya mahitaji yao tunaweza kusema maneno tunayokwisha kusema juu ya wazee. Kuna watumishi wengine wanaofanya kazi ya mshahara, na hivi wanajipatia mali wao wenyewe kwa mahitaji yao. Tena kuna wengine wanaoweka saa yao yote kwa kazi ya Mungu. Kwa watu namna hii inatupasa kutii maagizo ya Maandiko Matakatifu,

> "Wale wanaohubiri Habari Njema wapate maisha yao kwa Habari Njema" (1 Wakorinto 9:14).
>
> "Yeye aliyefundishwa katika neno, ashiriki naye aliyefundisha katika maneno yote yaliyo mema" (Wagalatia 6:6).

**4**. Halafu kwa kumaliza mafundisho yetu juu ya watumishi, tuangalie tena Wafilipi 1:1. Pale tunaona watu namna tatu katika kanisa la Mungu, watakatifu, waangalizi (au wazee) na watumishi. Hatuoni namna nyingine za watu kama pasteur, vivyo hivyo. Hatusomi juu ya mtu mwingine aliye kiongozi cha wazee na watumishi. Hivi tunajua ya kwamba kanisa linalojaribu kufuata utaratibu wa Neno la Mungu lina watakatifu, wazee na watumishi tu. Hakuna watu wa namna nyingine au **wenye jina lingine.**

# MALI YA KANISA

**1. Mali kwa kazi ya kanisa linatoka wapi?**

Katika Agano Jipya tunaona ya kwamba mali kwa kazi ya kanisa inatoka kwa Wakristo wale wanaokaa katika kanisa lile. Mali ya wasioamini haiwezi kutumika kazi ya Mungu. Kutoa ya mali yetu kwa Bwana ni sehemu ya kuabudu kwetu, hivi ni kwa wale tu wanaokwisha kukombolewa na damu ya Kristo kutoa mali kwa kazi ya kanisa. Wala hatuoni ya kwamba kanisa moja linapata kusaidiwa kila mara na mali kutoka kwa kanisa lingine au pahali po pote pengine. Sharti Wakristo wa kanisa fulani watoe mali ya kufaa kwa kutembeza kazi ya kanisa lao. Wakati tunapofikiri juu ya mali ya kanisa, tufahamu maneno haya:

A. **Mali yote Mkristo aliyo nayo ni mali ya Mungu.** Mungu alimpa mali hii ili atumike nayo kwa utukufu wa Bwana. (Ona Luka 16:1-12). Haifai sisi kuvimbisha mali ya Bwana kwa sisi wenyewe. Inatupasa kumpa yote tusiyohitaji kabisa kabisa kwa sisi wenyewe na nyumba yetu. Inatupasa kufikiri saa zote nini tunaweza kufanya na mali yetu itakayokuwa na faida zaidi kwa Bwana.

B. **Mkristo anaagizwa kutoa kwa kazi ya Bwana.**

1. **Atatoa wakati gani?** "Siku ya kwanza ya juma, kila mtu kwenu aweke akiba kwake" (1 Wakorinto 16:2).

2. **Atatoa ngapi?**

   **a.** "kwa kadiri ya mapato yake" (1 Wakorinto 16:2).

   **b.** Kama Kristo alivyotoa. Yeye alikuwa mtajiri lakini aligeuka masikini ili sisi tuwe watajiri (2 Wakorinto 8:9). Yeye ndiye mfano wetu.

   **c.** Inatupasa kutoa katika umasikini wetu, si mali ambayo ilituzidi tu (Marko 12:44).

   **d.** Inatupasa kutoa na ukarimu. Mwisraeli hakuweza

kutoa kidogo kuliko sehemu moja ya kumi, ndiyo zaka. Lakini alitoa zaka na **zabihu**. Inapasa Mkristo, aliye chini ya neema, kutoa kuliko sehemu moja ya kumi ya mapato yake kwa Bwana.

**3. Atatoa na roho gani?**

**a.** Ajitoe kwanza mwenyewe kwa Bwana (2 Wakorinto 8:5) na hivi kukiri ya kwamba mali yake yote ni mali ya Bwana.

**b.** Sharti aitoe kwa sababu ya mapendo. Kama sivyo, zawadi yake haina faida kwa Mungu (1 Wakorinto 13:3).

**c.** Inampasa kutoa zawadi yake kwa siri (Matayo 6:1-4), kwa siri kabisa hata mkono wake wa kushoto usijue nini mkono wa kuume unafanya. Huu ndio mfano.

**d.** Inapasa kutoa na furaha, si kwa huzuni (2 Wakorinto 9:7).

**e.** Tunaona ya kwamba Wakristo wa kwanza waliuzisha vita vyao vyote, na kugawa mali waliyopata kwa njia hii katikati yao (Matendo 2:44,45; 4:31-37). Huu ulikuwa mfano wa inje wa upatano wa roho zao na Mungu. Hatuagizwi kufanya hivi pahali pengine katika Agano Jipya. Zaidi mashairi ambayo yanatufundisha juu ya kutoa yanaonyesha ya kwamba mtu ana mali yake mwenyewe. Neno hili Wakristo wa kwanza walilofanya halikuwa sharti. Lilikuwa kitu kilichotoka kwa roho zao, ambacho walikifanya kwa mapenzi yao.

4. **Zawabu kwa wale wanaotoa ni nini?**

**a.** Kama tukitenda kwa uaminifu na mali ya uzalimu, ndiyo mali ya dunia, Mungu atatupa mali ya kweli, mali ya roho (Luka 16:11).

**b.** "Matunda yanayozidi kuwa mingi katika hesabu yenu" (Wafilipi 4:17). Atakuwa na hazina mbinguni (Matayo 6:19-21) kwa sababu zawadi zake ni "Harufu ya manukato, zabihu ya kukubaliwa inayopendeza Mungu" (Wafilipi 4:18).

**C. Wale wanaochunga mali ya kanisa sharti watumike nayo kwa utaratibu kabisa.**

**1.** "Kwa sababu tunatangulia kufikiri maneno yaliyo mema,

si mbele ya Bwana tu, lakini mbele ya watu" (2 Wakorinto 8:21). Sharti watu wawili au zaidi wachunge mali ya kanisa. Katika Matendo 6:1-6 tunaona ya kwamba walichagua watu saba kuangalia maneno ya kugawa mali kwa wajane katika kanisa. Barua za Agano Jipya hazionyeshi sharti wenye kuchunga mali ya kanisa kuwa hesabu fulani, lakini tunaona wazi kwa njia ya 1 Wakorinto 16:3,4 na 2 Wakorinto 8:18,19 ya kwamba ilikuwa desturi yao kuweka kazi hii mikononi mwa watu wawili au zaidi. Katika 1 Wakorinto 16:3,4 Paulo anasema ya kwamba atatuma wale waliokubaliwa na Wakristo wa Korinto na sadaka yao kwa Yerusalema, na kama ikihitajiwa atakwenda yeye mwenyewe vilevile. Katika 2 Wakorinto 8:18,19 Paulo anapasha ya kwamba ndugu mwingine alichaguliwa kusafiri pamoja naye kwa kupeleka zawadi kutoka kwa kanisa lile.

**2. Mali ya kanisa itatumika kazi gani?**

Agano Jipya linaonyesha zaidi njia kubwa tatu. Kuna wajane katika makanisa wanaohitaji kuchungwa, kuna watakatifu wamasikini, na kuna wale wanaotumika saa yao yote juu ya kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu.

**A. Kwa wajane katika kanisa** (Matendo 6:1-6). Kwa mwanamke kuhesabiwa kama mjane wa kweli (1 Timoteo 5:3-16), ilimpasa kutimiza maneno haya:

1. Sharti awe pekee kabisa, au kusema bila ndugu wanaoweza kumsaidia, mwanamke anayelazimishwa kutegemea kweli Bwana tu kwa mahitaji yake (mash. 4,5,16).
2. Sharti awe na miaka 60 au zaidi.
3. Sharti ajulikane kwa sababu
   a. ya kazi njema
   b. alilea watoto wake vizuri
   c. alipokea wageni na furaha
   d. alikuwa na roho ya mapendo na ya kusaidia kwa watu wengine (sh.10).

**B. Kwa watakatifu masikini.** Mungu anatuonya mara nyingi katika Neno Lake kukumbuka wamasikini. Ona Wagalatia 2:10; Waroma 12:13. Katika Agano la Kale tunaona ya kwa-

mba Waisraeli wale waliokumbuka ndugu zao masikini walisitawi kabisa wao wenyewe (Torati 14:29).

Kama miaka 45 nyuma ya kuzaliwa kwa Kristo, Wakristo wengi katika Yudea walikuwa masikini kabisa. Tunazani ilikuwa kwa sababu ya mateso makali waliyopata kwa sababu ya imani yao na kwa sababu njaa ilikuwa inchini. Watakatifu wa Antiokia walituma mali kusaidia ndugu zao kwa Yudea kwa mikono ya Barnaba na Saulo (Matendo 11:27-30). Kanisa kwa Korinto walipewa maonyo kufanya vivi hivi (1 Wakorinto 16:1-3; 2 Wakorinto 8 na 9). Ni kazi yetu vilevile kuchunga wale walio na mahitaji. Bwana Yesu alisema, "Siku zote muna masikini pamoja nanyi" (Marko 14:7). Ni vizuri kwa kanisa kuwa na wengine katikati yao walio masikini waweze kushiriki pamoja kuwasaidia.

Lakini si kazi ya kanisa kuchunga wale walio masikini kwa sababu wanakataa kutumika kazi. Mungu anasema kama mtu asipotaka kutumika asile chakula (2 Watesalonika 3:10).

**C. Kwa wale wanaoweka saa zao zote juu ya kazi ya Bwana.**

1. Wale wanaohubiri Habari Njema au kufundisha Neno la Mungu saa zote wanasitahili kusaidiwa na kanisa. "Lakini yeye aliyefundishwa katika neno, ashiriki naye aliyefundisha katika maneno yote yaliyo mema" (Wagalatia 6:6). Ona vilevile 1 Wakorinto 9:4-14 na 1 Timoteo 5:17,18.
2. Lakini mara nyingi Mtume Paulo alitumika na mikono yake kwani hakutaka kupokea mali kutoka makanisa (Matendo 18:3). Alifanya hivi kwa sababu
   a. Alitaka kuwa mfano kwa Waefeso, hata wao vilevile waweze kusaidia wazaifu na kujua baraka ya kutoa (Matendo 20:33-35).
   b. Kuzuiza watu wasiwe na njia ya kusema ya kwamba Paulo alikuwa akitumikia Mungu kwa sababu ya kupata mali katika kazi hii (2 Wakorinto 11:7-12).
   c. Hakutaka Watesalonika kuwa na mzigo wa kumsaidia na mahitaji yake (1 Watesalonika 2:9; 2 Watesalonika 3:7-9). Watakatifu pale kwa Tesalonika walikuwa masikini na waliteswa sana kwa sababu ya imani yao.

3. Kanisa kwa Filipi lilipata sifa kwa sababu ya kutuma mali kwa Paulo (Wafilipi 4:10-19). Ona ya kwamba Paulo hakutaka zawadi yao kwa sababu ya mahitaji yake mwenyewe, lakini kwa sababu alitaka wazae matunda kwa utukufu wa Bwana.

4. Ona vilevile ya kwamba hata kama Paulo hakusema kitu juu ya mahitaji yake mwenyewe, hakuogopa kujulisha wengine mahitaji ya watakatifu wengine (2 Wakorinto 8 na 9).

Hivi kwa kumaliza tunaona maneno makubwa mawili juu ya mali ya kanisa:

a. Ni kazi ya Wakristo kutoa ya mali yao mali ya kutosha kwa mahitaji ya kazi ya kanisa, bila kusukumwa, lakini na ukarimu na furaha.

b. Inapasa kanisa kutumika na mali hii kwa njia hizi tatu tunazokwisha kuonyesha. Haifai kanisa kuvimbisha mali.

# KAZI YA WANAWAKE

**1. Maandiko Matakatifu yanatufundisha waziwazi juu ya pahali pao na kazi yao katika kanisa:**

**A.** Mbele ya Mungu mwanamume na mwanamke wanaokolewa sawasawa na wanakubaliwa naye sawasawa. "Hapana mwanamume wala mwanamke. Maana ninyi wote ni mmoja katika Yesu Kristo" (Wagalatia 3:28).

**B.** Lakini kwa njia nyingine maneno ya wanaume na wanawake ni mbalimbali katika kanisa. Ona kwa mfano katika Waefeso 5: 22,25 maonyo haya:

"Ninyi wake, mutii waume wenu" (sh.22).

"Waume, mupende wake wenu" (sh.25).

Hivi tunaona ya kwamba mbele ya Mungu mwanamke anakubaliwa sawasawa na mwanamume, lakini katika kanisa la Mungu ni mwanamume aliye kichwa na kiongozi, na mwanamke ni kwa pahali pa kutii.

**2. Kutii huku kutaonekana kwa njia mbalimbali.**

**A. Mwanamke anaagizwa kunyamaza katika kanisa** (1 Wakorinto 14:34,35). Maana ya agizo hili inaonyeshwa kuwa hivi:

1. Haifai afundishe (1 Timoteo 2:12).
2. Haifai aulize maneno katikati ya watu wote (1 Wakorinto 14:35).
3. Inampasa kujifunza katika kimya akitii "kwa kila namna" (1 Timoteo 2:11).

**B. Haifai mwanamke kutawala mwanamume** (1 Timoteo 2:12).

**C. Haifai kwake kuomba au kutabiri wakati** kichwa chake kisipofunikwa (1 Wakorinto 11:5). Neno hili halisemi ya kwamba wanawake wanaweza kuomba na sauti katika kanisa kama wakifunika vichwa vyao kwani katika 1 Timoteo 2:8 tunasoma

"Ninataka **wanaume** waombe kila pahali."

**3. Kama maagizo haya yakisukumwa na nguvu juu ya wanawake,**

**A. Hawatayatii na furaha** lakini kwa sababu ni sharti, na Mungu hatapendezwa (Zaburi 51:17) .

**B.** **Roho za wanawake zitageuka chungu**. Lakini kama wakifahamu vizuri maana ya maagizo haya, na kuyatii na mapendo na kunyenyekea, wanafurahisha Bwana sana (1 Samweli 15:22).

**4. Mungu anakwisha kuonyesha katika Neno Lake kwa nini inapasa wanawake kutii wanaume.**

**A.** **Hata wakati wa kuumba dunia, Mungu aliumba mwanamume kwanza, kisha mwanamke** (1 Timoteo 2:13; 1 Wakorinto 11:8). Ni kama Mungu anataka kuchunga utaratibu huu aliosimamisha wakati wa kuumba dunia kuwa hivi katika kanisa vilevile, na tunasoma ya kwamba kichwa cha mwanamke ni mwanamume (1 Wakorinto 11:3).

**B.** **Kusudi la Mungu wakati alipoumba mwanamke lilikuwa awe msaidia wa mwanamume.** ″Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, lakini mwanamke kwa ajili ya mwanamume″ (1 Wakorinto 11:9).

**C.** **Zambi iliingia dunia wakati Hawa alipojaribu kutawala bwana yake,** "Adamu hakudanganywa, lakini mwanamke akidanganywa, aliingia hali ya kukosa" (1 Timoteo 2:14).

**D.** **Paulo anataja utaratibu ambao tunaona katika Agano la Kale ya kwamba wanawake walikuwa wenye kutii wanaume.** ″Watii kama sheria inavyosema vilevile″ (1 Wakorinto 14:34). Hata kama hatuoni agizo hili waziwazi katika Agano la Kale, tunaona ya kwamba walifanya hivi kila mara.

**E.** **Juu ya agizo kwa wanawake kufunika vichwa vyao,** tunaweza kusema maneno mawili mengine:

1. Malaika wanatazama. "Kwa sababu hii imepasa mwanamke awe na alama ya utii kwa kichwa chake, kwa ajili ya malaika" (1 Wakorinto 11:10). Shairi hili linaonyesha majeshi ya malaika wakitazama utaratibu wa Mungu hapa duniani, na ya kwamba wanaume ndio viongozi. Hivi malaika wanaona ya kwamba zambi Hawa aliyofanya haifanywi tena katika kanisa vilevile.
2. Namna wanawake walivyoumbwa inaonyesha neno hili vilevile. "Sheria ya asili yenyewe haiwafundishi ninyi, ya kwamba kama mwanamume akiwa na nyole ndefu, ni haya kwake? Lakini kama mwanamke ana nyole ndefu, ni utukufu kwake" (1 Wakorinto 11:14,15). Wakati Mungu alipoumba mwanamke alimpa kitu cha kufunika nacho, ndicho nyole ndefu. Paulo anasema hapa ya kwamba neno hili linaonyesha ya kwamba inapasa wanawake kufunika vichwa vyao wakati wanapoomba au kutabiri.

**5. Wakati tunaposema ya kwamba inapasa wanawake kutii wanaume, labda wengine watafikiri wanawake hawana kazi kufanya katika kanisa.**

Lakini sivyo. Maandiko Matakatifu yanaonyesha kazi namna mbalimbali.

**A. Kazi yake moja ni kuzaa watoto na kuwalea kwa Bwana** (1 Timoteo 2:15). "Ataokolewa" katika shairi hili, maana yake haiko kusema mwanamke akizaa watoto roho yake itaokolewa. Vilevile maana yake haiko kusema hatakufa wakati wa kuzaa. Maana yake ni kusema ya kwamba yeye vilevile ana kazi kubwa. Kama yeye na mume wake wakidumu katika njia ya Bwana, labda siku nyingine atakuwa na wana watakaohubiri Habari Njema. Hivi mwanamke si bule, lakini ana kazi hii kubwa kulea watoto wake kwa Bwana.

**B. Tunaona kazi nyingine wanawake waliyofanya katika Agano Jipya.**

1. Walitoa ya mali yao (Luka 8:3).
2. Walipokea wageni vizuri (Waroma 16:1,2).
3. Walifundisha wanawake vijana (Tito 2:4).

Watu wengine wanajaribu kubisha maagizo haya kwa wanawake kwa njia mbalimbali. Wanasema:

1. Mafundisho ya Paulo juu ya maneno haya yanaonyesha ya kwamba hakupenda wanawake, na hatusikii vilevile ya kwamba alioa mwanamke yeye mwenyewe. Utawajibu hivi:

   Paulo anasema ya kwamba mafundisho yake yanatoka kwa Roho Mtakatifu, na ni "agizo la Bwana" (1 Wakorinto 14:37).

2. Paulo alikuwa akifundisha tu kitu kilichokuwa desturi kwa wakati ule na maneno haya si kwa wakati wa sasa. *Jibu:*

   Paulo hakuandika barua yake ya kwanza kwa Wakorinto tu, lakini kwa "wote wanaoitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo katika kila pahali" (1 Wakorinto 1:2). Hivi maagizo haya ni kwa makanisa yote.

3. Katika 1 Wakorinto 11:16 Paulo anasema ya kwamba maneno haya si sharti, na ya kwamba desturi namna hii hazikutendwa katikati ya makanisa. *Jibu:*

   Kueleza shairi hili hivi ni kusema Maandiko Matakatifu hayakuandikwa na Mungu. Maana ya shairi hili ilikuwa ya kwamba watu hawakubishana juu ya maagizo ya Bwana

katika makanisa. Makanisa yaliyakubali na kuyatii.

4. Kama mwanamke alipewa nyole ndefu kuwa kifuniko, kwa nini anahitaji tena kifuniko kingine? *Jibu:*

   Katika 1 Wakorinto sura 11 tunaona vifuniko namna mbili. Tunaona nyole zake kama kifuniko katika shairi 15, lakini tunaona kifuniko kingine katika shairi 5. Kama sivyo, shairi sita halina maana, kwa kusema:

   > "Kama mwanamke asipovaa nyole zake anyolewe. Lakini kama ni haya kwa mwanamke kunyolewa, avae nyole zake."

   Kila mtu ataona wazi ya kwamba neno hili halifahamikani. Hivi tunaona wazi ya kwamba mwanamke anahitaji kifuniko kingine, si nyole zake tu.

**C. Maana ya agizo kwa wanawake kunyamaza katika kanisa** (1 Wakorinto 14:34) ni kusema wasisemeseme au kuzungumuza wakati mtu anapohubiri?

Hapana. Neno linalotumiwa hapa kwa "kusema" katika Kiyunani si neno linalotumiwa kwa mazungumzo bulebule. Ni neno lililotumiwa vilevile katika shairi 21, "Nitasema na watu hawa, kwa watu wa lugha nyingine."

Kuna maulizo mingi mengine juu ya pahali pa mwanamke katika kanisa. Ni vizuri kwa mwanamke kutoa ushuhuda wake katika kanisa, au kupasha juu ya kazi yake kwa Bwana? Kama hakuna mafundisho waziwazi ndani ya Agano Jipya juu ya neno lenyewe, ni vizuri tujiulize:

1. Mwanamke akifanya kitu hiki, atatawala mwanamume?
2. Mwanamke akifanya kitu hiki, anatenda kama kiongozi?
3. Mwanamke akifanya hivi, anafundisha Neno la Mungu kwa wanaume?

Kama jibu ni "Ndiyo," haifai mwanamke kufanya neno hili.

**7. Mungu alitoa maagizo haya kwa kutusaidia sisi watu na kwa utukufu Wake vilevile.**

Pahali watu wasipochunga utaratibu huu, kuna magomvi na machafuko. Zaidi ya dini namna namna za uwongo zilianzwa kwa njia ya wanawake.

Lakini ni kitu kitamu sana kuona wanawake Wakristo wakichunga pahali pao pa kunyenyekea katika kanisa, na wakionyesha "roho ya upole na utulivu iliyo ya damani kubwa mbele ya Mungu" (1 Petro 3:4).